
MACHI-APRIL MMXXV - TOLEO LA LI

# NGURUMO

*ya Mwandishi*





## AMANI NI TUNU

**HABARI KUU:**

•VITABU VYA WASHINDI WA TUZO NYERERE MSIMU WA PILI VYACHAPWA

# YALIYOMO




**JALADA**

**Laura Pettie na Dkt. Aneth Komba (TET)**

Safari ya Malezi - 09
Kanuni Bora za Malezi
Uk wa 24 na 25

**MWANDISHI WETU**
David Yuvent Kisesa — 03

**PITIO LA VITABU**
Chungu Tamu — 06 — 05

**SAIKOLOJIA**
Wewe ni Kile Unachozalisha — 06

**MAKALA**
Kusoma, Tiba ya Msongo wa Mawazo — 08

**HABARI MOTO**
Vitabu vya Washindi Tuzo Nyerere Vyazinduliwa — 17

**KUTOKA MAKTABA**
Elvis Estabulus Musiba — 23

**HADITHI: Uk - 12 - 13, 14 - 15, 26 - 27 na 28 - 29**

**DAWATI LA WATOZI**

**+255 766974865 -** WHATSAPP

**+255 672 160 016** Piga

Richard Mwambe

## MWANDISHI WETU:

**David Yuvent Kisesa**

**Katika safu yetu ya Mwandishi Wetu, leo tupo mezani na kijana, mwandishi machachari wa kizazi cha sasa cha kifasihi. Najua una kiu ya kumjua, usihofu, huyu hapa. Si mwingine ni David Yuvent Kisesa au mwenyewe hujiita 'Sadari Kisesa'.**




**Sadari Kisesa**

Naitwa David Yuvent Kisesa, jina la uandishi ndiyo hilo 'Sadari Kisesa'. Wengi mnajiuliza jina Sadari limetokea wapi?... Jina hilo limetokea Morogoro, watu wa Morogoro wameniita jina hilo baada kuona muda mwingi nakaa na wahuni napiga nao stori sana na wahuni wananisikiliza wakajua mimi ndio sadari wao ambao nawauzia bangi wale wahuni, ilo jina ndio likakua namna hiyo.

Mimi ni mtoto wa kwanza wa Mzee Kisesa. Nimezaliwa tarehe 17/05/1997 katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, jijini Dar es salaam. Elimu yangu ya msingi nimeipata ale Shule ya Msingi Makuburi iliyopo Mabibo. Na nikabahatika kupata elimu ya sekondari kwenye Shule ya Sekondari Yussuf Makamba, nayo ipo hapohapo Mabibo.

'Shule ya wanajeshi' nasema hivyo kwasababu ipo jirani na kambi ya jeshi, nimesoma mpaka kidato cha nne sikwenda mbele kutokana na matokeo yangu ya kidato cha nne kufungiwa kwasababu ya kutolipwa pesa ya mtihani wa mwisho NECTA. Nikaachana na elimu mwaka 2014 nikaenda Morogoro kushika jembe. Mtajiuliza kwanini Morogoro?

Morogoro ndipo wanapotoka wazazi wangu, kwahiyo mimi Mluguru kindakindaki wa Mgeta. Kuanzia mwaka 2015 mpaka mwaka 2016 nililishika jembe nika-*deal* na kilimo cha biashara cha Nyaya sijaona mafanikio, ikabidi nirudi Dar es salaam kutafuta maisha kwenye mkoa niliozaliwa. Mwaka huo 2016 ndiyo nilioanza uandishi. Ilikuwa ghafla tu nilipenda kuandika baada ya kuingia mitandaoni na kuona vijana wakichuana kwa kasi katika tasnia ya uandishi bunifu.

Kwasasa nina miaka 29 sijafikiria kuacha kuandika nitaandika mpaka mwisho wa uhai wangu.

Kama nilivyosema awali nimependa uandishi kwa sababu ya kuona vijana wenzangu wanavyotikisa mtandaoni na uandishi wao, nikavutiwa na mimi nikaona nijiunge nao huko nipambanie kombe japo ulikuwa hauna faida yoyote zaidi ya kuburudisha mashabiki tu.

Kwakweli kuna changmoto nyingi sana kwenye uandishi kwa sababu humohumo utakutana na wezi, wajuaji wa mambo na chuki n.k.

Mimi bado sijachapa kitabu cha kuingia sokoni bali nilichapa kitabu nakala moja tu kwa ajili ya kuwaburudisha jamii inayonizunguka.

Malengo ni mengi kama mwandishi natamani kuchapa vitabu, simulizi zangu zisikilizwe na zitumike hata kwenye nyanja ya filamu na tamthilia.

Kwa anayependa kazi zangu, nyingi zipo Youtube kwenye *channel* yangu ya UKAE MEDIA zimesimuliwa kwa njia ya sauti.

Nyingine zipo kwenye akaunti yangu ya Facebook ya Sadari Kisesa zimeandikwa na zipo tayari kwa kusomwa, kama shabiki anahitaji kuburudika na Sadari Kisesa fuata hayo majina tajwa ataburudika kwasababu daima sina kazi mbovu.

### SADARI KISESA

Ni moja ya waandishi wanaokuja kwa kasi katika tasnia ya uandishi bunifu.

Katika mtandao wa Facebook kalamu yake inaandika kwa wino wenye mashiko. Na kule Youtube 'UKAE MEDIA' utazisikiliza kwa sauti tamu simulizi zake.

Msomaji na msikilizaji kqazi kwako. Msome umjue!

**GIZA GIZANI**

**Na Frank James Slaa**




Ndewande ni kijana aliyeishi akililia mwanga wa ndoto zake, lakini kila mlango wa maisha ulimfungia gizani. Elimu aliyopigania kwa damu na machozi haikumtoa kwenye minyororo ya umaskini, badala yake ikamzika kwenye mzigo wa matarajio yasiyo na ukomo.

Kadri siku zinavyosonga, heshima inabadilika kuwa kejeli, upendo wa familia kuwa kisu moyoni na matumaini kuwa moshi unaopotea angani.

Katika mzunguko huu wa kukata tamaa, je, ataibuka na mwanga wa kesho au atamezwa kabisa na giza lisilo na mwisho?

**Jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu**

Kinapatikana wapi?

Posta Mpya kwa George - 0755454152

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - 0655428085

Arusha kwa Ally Saidi - 0757690302

Konzo Bookshop Mafinga - 0763714862

Morogoro na Dodoma - 0687341398

DIWANI YA CHUNGU TAMU

MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI

WACHAPISHAJI: TPH

MWAKA: 1985

*Inatoka toleo lililopita…*

Hivyo mwandishi anaitaka jamii itakayojengwa iepukane daima na suala la vita.

**7. SUALA LA MAPENZI**

Mwandishi amejadili aina mbali mbali za mapenzi katika diwani hii kama ifuatavyo;

Mosi,mapenzi ya mtu na nchi yake.Haya mapenzi tunayaona katika shairi la “Daktari Askari” ambapo tunona kuwa,wakati wa vita kati ya Uganda na Tanzania raia,wanajeshi,manesi,n.k.walijitolea kwa moyo wa dhati kwenda kupigana ili kuikomboa nchi yao.Mapenzi haya ni ya kweli na dhati.Mapenzi ya Iddi Amini Dada kwa nchi yake hayakuwa ya dhati ndiyo maana alitumia mabavu kuiongoza nchi yake.


Pili, Mapenzi mengine kati ya mtu na nchi yake yanapatikana katika shairi la“Ngulu Wapaona”Katika shairi hili msanii anaonesha umuhimu wa kuwa na mapenzi na kwenu (nchi yako) hata kama ni porini. Msaanii anamtaka kila mtu kuthamini kwao hata kama kuna karaha.Anaonesha kuwa kwenu ni kwenu na ukuthamini na kukuheshimu kwa raha na Baraka.

Tatu, mapenzi kati ya mwanamume na mwanamke. Mapenzi haya mwandishi ameyagawa ktika makundi makuu mawili ya mapenzi ya dhati na yale ya udanganyifu.Mashairi yanayoongelea mapenzi ya dhati ni yale ya “Daktari Askari”, “Thomas na Doto”,“Manzese Mpaka Ostabei” pamoja na lile la “Takukumbuka Daima.” Mashairi yanayoongelea mapenzi ya udanganyifu ni kama vile “Usiwe Mwonja Asali”, “Fikra za Waungwana”.

Mapenzi ya dhati ni ya kuheshimiana,Mapenzi yasiojali hali au kipato cha mtu. Mapenzi ya uaminifu. Mapenzi kati ya Daktari Adam na Eva katika shairi la “DaktariAskari” yalikuwa ya dhati, bila kujali kwao au utaifa.Hali kadhalika mapenzi kati ya Thomas na Doto yalikua ya dhati bila kujali rangi au taifa.Na mapenzi kati ya Mashaka na Dorothy yalikuwa ya dhati bila kujali pesa au utajiri. Mapenzi ya dhati husababisha uvumilivu katika maisha.Mapenzi ya dhati huzaa matunda mema katika ndoa,yaani hujenga ndoa za uaminifu.Hivyo mapenzi ya dhati huzaa ndoa za kudumu,ndoa zisizojali rangi,utajiri,utaifa au hali ya mtu.Ndoa za uaminifu zilizotokana na mapenzi ya dhati Katika diwani hii ni zile kati ya daktari Adam na Eva, pamoja na ile ya Mashaka na Dorothy.

Mapenzi ya udanganyifu nayo pia huzaa ndoa za udanganyifu na mara nyingi ndoa hizo huwa hazidumu.Katika shairi la “Usiwe Mwonja Asali”,msanii anaonesha jinsi mapenzi ya udanganyifu yanavyosababisha uchumba wa udanganyifu.Msanii anaishauri jamii kuwa ukiwa na mchumba msiwe na tabia za kujamiiana ovyo,bali mpaka mtakapooana.

Katika shairi la “Fikra za Waungwana” mwandishi anadhihirisha wazi jinsi mapenzi ya udanganyifu yanavyosababisha ndoa za ulaghai. Mwandishi anasema:-




“Mume wangu nakupenda, Joseph amenikuna,

Nimekula naye tunda, ninampenda sana,

Na usifanye inda, mimi ni wako kimwana,

Nitaishi kwa mpango, kwako na kwake Joseph.”

Kwa ujumla mwandishi anaitaka jamii yetu idumishe mapenzi na ndoa za dhati.

*Itaendelea toleo lijalo...*

## WEWE NI KILE UNACHOZALISHA



**Madam Neema Mgao**

WEWE NI KILE UNACHOZALISHA

U hali gani mpendwa rafiki yangu, ni matumaini yangu kuwa upo salama. Ikiwa kuna changamoto zozote nikusihi usivunjike moyo wala kukata tamaa kwani changamoto ndio uimara wa akili. Akili ya binadamu inakuwa imara na muda wote inakua tayari kuchanganua mambo na kuyatekeleza ipasavyo. Changamoto ndio kipimo cha utashi wa mwanadamu.

Katika makala ya saikolojia kwenye toleo hili nitaongelea ni namna gani ya kuwa vile unachojizalishia kuwa.

Wewe ni kile unachozalisha, kisaikolojia na kimaisha ya kawaida unaishi vile unavyokua na kujitengeneza kuwa. Unapokaa na kuwaza mawazo yako na eidha kuyatimiza yaani kuyakamilisha mawazo au ukayawaza na ukayaachia njiani ndivyo mambo huwa. Yale mawazo unayoyawaza ndio kwa asilimia kubwa yanakuja kutimizwa na vile unavyoishi. Umewahi kuwaza kuwa ifikapo siku ya Jumanne utafanya jambo fulani na pengine ukaliandika kabisa, ukilikamilisha kwa kulitenda siku husika utaona unapata amani na utajihisi kuwa umekamilisha jambo hilo. Inaweza kutokea lile jambo haujalitimiza, utapata hali kama ya fadhaa moyoni na unaweza kujihisi kama una deni.

Wewe ni kile unachozalisha, mfano; vyumba viwili vya giza, halafu kukafanyika majaribio ya mwanga kuwekwa katika vyumba hivyo. Chumba cha kwanza, ikachukuliwa tochi ikawekwa kwenye kona ya chumba ikiwa imelazwa chini, fanya jaribio hilo na utagundua au utaona kuwa mwanga utaakisi upande wa pili na chumba kitakua na mwanga kiasi huku kukiwa na uwezekano wa giza kubaki upande torch ilipo. Hii ni sawa na kusema kuwa, kuna wakati kwenye maisha unaweza usifaidike na yale uyafanyayo, kwamba unaweza kuwa taa kwa wengine huku kwako ukibaki giza, hii ikupe nguvu ya kujitoa kwa kiasi huku ukijikumbuka.

Jaribio la pili, chumba cha pili chenye giza pia, weka tochi katikati ya chumba kisha isimamishe mwanga upige juu darini, matokeo yake utaona ni kuwa chumba chote kitaenea mwanga, hivyo tutapata mwanga kwakuwa tochi imepiga juu ya dari na chumba chote kitaangaza mwanga. Ndivyo ilivyo kwenye maisha yako ya kila siku, ili uwe wewe na uishi maisha vizuri na uone matunda au matokeo chanya katika maisha yako basi huna budi kuzalisha nguvu chanya kulingana na vile unavyotakiwa uwe.

Vile unavyoishi na shughuli uzifanyazo hakikisha kuwa mnufaika wa kwanza wa shughuli uzifanyazo iwe ni wewe mwenyewe. Ikiwa un-

afanya shughuli fulani katika jamii hakikisha unajikumbuka, usifanye mambo yatakayopelekea kujisahau. Hatuwezi kupata uhai kwenye kukata tamaa kwako, yaani ili jamii istawi inakupasa wewe utoe nguvu chanya za kustawisha jamii inayokuzunguka. Wewe ni kile unachotuonyeshea kuwa upo hivyo. Inakupasa uweke juhudi kwenye kujiimarisha kuwa wewe ili tupate nguvu chanya kwako.

Wewe ni kile unachozalisha, ikiwa una huruma sana basi tukuone ukitenda matendo mema.
Wewe ni kile unachozalisha, hatuwezi kuzungukwa na watu wenye roho mbaya ikiwa wanatuonyesha wema. Kama wana ubaya mioyoni mwao ni humo ndani mwao ila ikiwa hadharani wanatuonyesha kujali, huruma, kutupenda basi ni wazi kuwa nguvu chanya ndio itatawala kuliko ubaya wao wa moyoni. Kile kinachozalishwa kikatoka nje ndio uhalisia wa mambo husika.

Vile uwavyo na ndivyo wakuzungukao huwa, kuna uwezekano mkubwa sana wa kupata watoto wakiwa na matusi na lugha chafu midomoni kwani wamelelewa na kukuzwa na mlezi au mzazi aliyetawaliwa na lugha ya matusi mdomoni. Kuna uwezekano mdogo sana wa kupata watoto wapole kutoka kwa mzazi au mlezi mwenye lugha ya matusi.

Katika fikra zako unajiona kuwa ni mwenye nguvu na mshindi wa changamoto zako zikuzungukazo. Picha ile iliyopo ndani ya fikra zako kuna uwezekano mkubwa sana wa saikolojia yako kuileta picha ile mbele ya uso wako na kweli hata tembea yako ikaonyesha kuwa wewe ni mshindi.

Ndio maana hata wagizaji wengi hufanikiwa kuigiza jambo fulani kwani huuvaa uhusika na kupokea hali ya kimapokeo ya kile alichomezeshwa katika fikra zake. Ameambiwa kuwa "chukulia wewe ni mgonjwa", na kweli akalegea kabisa na kuonekana ni mgonjwa, basi mtu huyu anakuwa amevaa na amashibisha ubongo wake kuwa yeye ni mgonjwa na basi ubongo nao ukatoa nishati za kuulegeza mwili kiasi akawa mgonjwa kweli, ni elimu hii ndio imekua ikitumika. Hivyo, hivyo ulivyo au hivi nilivyo ni vile ubongo wangu umezalisha nguvu ya kuwa hivi nitakavyo. Kwa hivyo asilimia kubwa ya watu walivyo ni vile ambavyo ubongo umepokea na kutengeneza nguvu ya kuwa hivyo.

WEWE NI VILE UMEJIZALISHA NA KUJITENGENEZA KUWA. UKITAKA USHINDI, SHINDA KUANZIA KICHWANI MWAKO, KWAHIYO UKISHINDWA BASI UTAKUA UMESHINDWA KUANZIA KWENYE FIKRA ZAKO. JITENGENEZEE KUWEZA NA KUSHINDA, NA IWE HIVYO HUKU MUNGU AKIKUWEZESHA.

Hadi wakati mwingine katika makala nyingine ya saikolojia katika toleo lijalo.

Kwa huduma za vitabu na ushauri wa kisaikolojia wasiliana nami MADAM NEEMA MGAO kupitia +255763013206, napatikana DODOMA, TANZANIA.

Karibu sana.

official KITABU Market
www.kitabumarket.co.tz

**MAKALA**
**Na. Richard Mwambe**

# USOMAJI, TIBA YA MSONGO WA MAWAZO

USOMAJI wa vitabu ni miongoni mwa njia bora na zenye ufanisi mkubwa katika kukabiliana na msongo wa mawazo *(stress)*. Tafiti nyingi za kisaikolojia zinaonyesha kuwa kusoma kunaweza kupunguza msongo wa mawazo kwa hadi 68% ndani ya muda mfupi sana.

Zifuatazo sababu kuu zinazofanya usomaji kuwa tiba:

**1. Kumpumzisha Akili na Mwili**

Unapozama kwenye kitabu, akili yako inahamia kwenye ulimwengu mwingine. Hii inasaidia kupunguza mapigo ya moyo na kulegeza misuli iliyokaza kutokana na wasiwasi. Hata dakika sita tu za usomaji wa kina zinaweza kutosha kuanza mchakato huu wa utulivu.

**2. "Bibliotherapy" (Tiba ya Vitabu)**

Hii ni mbinu ya kitaalamu ambapo vitabu hutumika kusaidia watu wenye changamoto za kihisia. Kusoma kuhusu wahusika wanaopitia matatizo yanayofanana na yako kunaweza kukupa hisia ya kutokuwa peke yako na kukupa mbinu mpya za kutatua matatizo.

**3. Kuhamisha Makini (Distraction)**

Msongo wa mawazo mara nyingi hutokana na kufikiria sana matatizo ya sasa au yajayo. Vitabu vya hadithi *(fiction)* au fasihi simulizi husaidia kuishughulisha akili na mambo chanya, hivyo kuipa akili "likizo" kutoka kwenye vyanzo vya msongo.

**4. Kuboresha Usingizi**

Kusoma kitabu kilichochapishwa ***(sio cha kwenye simu)*** kabla ya kulala husaidia ubongo kutulia na kujiandaa kwa usingizi mzito. Usingizi bora ni nguzo muhimu katika kudhibiti msongo wa mawazo.

**Vitabu gani hufaa?**

Ili kupata matokeo bora, uchaguzi wa kitabu ni gani cha kusoma ni muhimu:

**Riwaya na Hadithi za Kubuni:** Hizi ni nzuri sana kwa ajili ya "kutoroka" kidogo kwenye uhalisia unaokupa msongo wa mawazo.

**Vitabu vya Maendeleo Binafsi** (*Self-help*): Hivi hukupa maarifa ya jinsi ya kuelewa hisia zako na mbinu za kukabiliana na changamoto.

**Mashairi au Maandiko ya Kidini/ Kiroho:** Husaidia kuleta amani ya ndani na tafakari ya kina.

**Kidokezo:** Ikiwa unahisi msongo umezidi uwezo wako, ni vyema pia kuzungumza na mtaalamu wa afya ya akili. Lakini kama hatua ya kwanza ya kila siku, kitabu ni rafiki wa kweli wa afya yako ya akili.

**Watu kadhaa wanaoshuhudia juu ya Tiba ya Vitabu(Bibliotheraphy)**

Watu wengi mashuhuri na wa kawaida wamewahi kukiri kuwa vitabu viliwaokoa katika vipindi vigumu vya msongo wa mawazo, sonona *(depression),* na upweke. Hapa kuna mifano michache ya watu ambao ushuhuda wao umesaidia kueneza dhana ya *'Bibliotherapy'* (Tiba ya Vitabu):

**1. Matt Haig**



Mwandishi huyu maarufu wa Uingereza amekuwa muwazi sana kuhusu mapambano yake na ugonjwa wa sonona na wasiwasi (anxiety). Katika kitabu chake cha *Reasons to Stay Alive*, anaelezea jinsi kusoma vitabu kulivyomsaidia kurudisha matumaini wakati akili yake ilipokuwa imevurugika. Kwake, vitabu vilikuwa kama "ramani" ya kumtoa kwenye giza.

**2. Oprah Winfrey**



Oprah amewahi kusema mara

nyingi kuwa vitabu vilikuwa njia yake ya kutoroka kutoka kwenye mazingira magumu na maumivu ya utotoni. Anashauri kuwa kusoma kunampa mtu uwezo wa kuona maisha nje ya matatizo yake ya sasa, jambo ambalo hupunguza shinikizo la kisaikolojia.

**3. J.K. Rowling**



Mwandishi wa mfululizo wa hadithi za *Harry Potter* aliandika hadithi hizo wakati akipitia kipindi kigumu cha msongo wa mawazo na umaskini. Anasema kuwa uandishi na usomaji wa fasihi vilimsaidia kuelezea hisia zake (kama vile wahusika wa *'Dementors'* ambao wanawakilisha sonona) na hatimaye kupata nafuu ya nafsi.

**Mifano halisi na tafiti za kitaalam**

Mbali na watu maarufu, kuna ushahidi wa makundi ya watu ambao wamepona au kupata nafuu:

**Wafungwa Magerezani:** Miradi mbalimbali ya vitabu magerezani (**kama Reading for Rehabilitation**) imeonyesha kuwa wafungwa wanaosoma vitabu hupunguza kiwango cha hasira na msongo wa mawazo, na kupata mtazamo chanya wa maisha baada ya kifungo.

Mmoja wa wasomaji nguli wa vitabu hapa Tanzania anashuhudia mara kadhaa kwenye mitandao ya kijamii jinsi gani yeye husaidia wafungwa gerezani kuweza kupata na kusoma vitabu. Anasema kuwa wafungwa hawahufurahi sana na mabadiliko chanya hujitokeza kwao.

**Wastaafu na Wazee:** Tafiti nchini Uingereza kupitia shirika la **The Reader** zimebaini kuwa vikundi vya usomaji wa pamoja vimesaidia wazee wengi kupona upweke na msongo wa mawazo unaotokana na uzee.

Hata hapa kwetu Tanzania, wapo watu wengi sana ambao wameweza kuondokana na msongo wa mawazo kwa usomaji wa vitabu. Mfano hai ni mwandishi wa makala hii, kipindi fulani katika maisha yake alipitia msongo mkubwa wa mawazo ambao wengi hawakuweza kuugundua. Anashuhudia kwamba hakujua hata nini anafanya hapa duniani. Lakini alipoirejea tabia yake ya usomaji wa vitabupasi na kujua kuwa itamletea uponyaji, alijikuta baada ya muda mfupi anapata matumaini mapya. Vitabu vilikuwa dawa yake kuu ya kumrudisha katika ulimwengu wa kawaida.

**Kwa nini "watu hupona"?**

Watu hawa hawaponi kwa "uchawi," bali kwa sababu ya mambo mawili makuu:

1. **Kujitambua *(Identification)*:** Unapoona mhusika kwenye kitabu anapitia maumivu kama yako na anashinda, akili yako inapokea ujumbe kuwa "**hata mimi nitaweza**."

2. **Mabadiliko ya Kikemia:** Kusoma vitabu vya vichekesho au hadithi za kusisimua hupunguza homoni ya *Cortisol* (inayoleta stress) na kuongeza *Dopamine* (inayoleta furaha).



# SHERIA NANE ZA HADITHI NZURI

**Na: Maundu Mwingizi (fb)**

Mnamo mwaka 1999, mwandishi Kurt Vonnegut–aliyeandika zaidi ya hadithi fupi 100–alifunua siri ya kuandika hadithi nzuri kwa kuandika sheria zake 8:

1. Usimpotezee muda msomaji wako.

– Kla neno unaloandika lazima liwe na thamani. Usijaze maelezo marefu ya mandhari au mazungumzo yasiyo na tija. Msomaji hana muda mwingi, hivyo nenda moja kwa moja kwenye kiini cha hadithi, vinginevyo utampoteza.

2. Mpe msomaji wako mhusika (character) atakaye mkubali/muunga mkono.

– Hata kama mhusika wako si mwema (muovu/adui), bado ni lazima awe na kitu kinachomfanya msomaji atamani kumwona akikifikisha mwisho. Hakikisha msomaji wako anakuwa na wahka/mshawasha wa kushuhudia mhusika huyo akianguka au akisimama imara.

3. Kila mhusika (character) anapaswa kutaka/kuhitajia kitu fulani. Hata kama ni glasi ya maji tu.

– Mhusika wako anataka nini? Anataka kuua au kuokoa? Anataka kuroga au kutibu? Hitaji hilo ndilo linalosukuma mhusika kufanya maamuzi–na hiyo ndiyo injini ya hadithi. Ikiwa mhusika hana analopambania kufanya, *my friend*, hakuna hadithi hapo.

4. Kila sentensi lazima iwe inafunua tabia ya mhusika au inaliendeleza tukio kwenye hadithi.

– Siku zote, msomaji hutaka kujua tukio linalofuata au walau kumjua zaidi mhusika (character) anayemfuatilia. Sasa kama sentensi haionyeshi msomaji mhusika ni mtu wa namna gani, na pia hailipeleki tukio mbele zaidi, ifute.

5. Anzia (kuandika) karibu na mwisho wa hadithi kadiri inavyowezekana.

– Kama hadithi yako itaanza kunoga kuanzia ukurasa wa hamsini, jiulize, hizi kurasa 40 za awali zina umuhimu gani? Usianze na historia ndefu ya kuzaliwa kwa mhusika ikiwa hadithi inahusu tukio la uzeeni. Ingia kwenye mgogoro wa hadithi haraka iwezekanavyo na uache maelezo yasiyo na lazima.

6. Kuwa mkatili. Yafanye mambo ya kutisha yawapate wahusika wako. Waache wasomaji waone wahusika hao wameumbwa namna gani (msimamo wao).

–– Katika hali halisi ya maisha, binaadamu hupitia mambo magumu na yenye kuumiza *(kama vile maradhi, vifo, majanga, kufutwa kazi, nk),* hivyo ukiwapitisha wahusika katika tanuri la changamoto za kimaisha na kuwaacha wajipambanie unawafanya wawe hai. Ukiwalinda sana wanapoteza uhai na uhalisia.

7. Andika kwa ajili ya kumridhisha mtu/msomaji mmoja tu.

– Kuna msemo usemao, rafiki wa wote si rafiki wa yeyote; huwezi kuwaridhisha watu wote wakati wote. Na ukijaribu kufanya hivyo utawaudhi na kuwapoteza wote. Chagua mtu (au kundi mahsusi), ambaye, utaandika kana kwamba unamsimulia yeye pekee. Hii inafanya hadithi iwe na hisia za dhati.

8. Wape wasomaji wako taarifa nyingi kadiri inavyowezekana na kwa haraka iwezekanavyo.

– Hakuna kitu kibaya kama kuijaza hadithi yako matukio ya sadfa *(coincidence)* na *surprises*. Msomaji atahisi unamhadaa. Hakikisha kila ukurasa unampa taarifa fulani muhimu itakayokuja kumpa jibu mbeleni mwa hadithi.

Wakatabahu,

Maundu Mwingizi (Mwana Balagha)

# SAKO KWA BAKO:

## EMMANUEL MOSES KINDOLE (MARUDIO)

**Happy birthday kwa mtaalamu wetu wa ma-graphics… huyu ni nani?**


Jina langu halisi naitwa Emmanuel Moses Kindole. Nakumbuka wakati nipo shule ya msingi, darasani mwetu kulikuwa na wakina Emmanuel wengine kama wanne hivi, hivyo kufanya idadi yetu tuwe watano. Hii ikawa inaleta mkanganyiko baina yetu. Maana mwalimu au mwanafunzi mwenzetu alipoita jina la mmoja wetu tukajikuta wakina Emma' wote tumeitika kwa wakati mmoja. Wajina wangu walikuwa wanaifurahia sana ile hali, ila kwangu ilikuwa inaniudhi sana hata nikaondokea kujibadili jina (siyo official) na kuligeuza kuwa Kindo Emmanuel, hivyo nikadumu nalo hadi Leo.

Tangu nikiwa bwana mdogo nilikuwa napenda sana kusoma vitabu hasa vya simulizi, na ndoto yangu kubwa ilikuwa nije kuwa mwandishi ili maandishi yangu yawe maktaba, yaje yasomwe na vizazi hata vizazi. Hivyo nilijifunza fasihi kwa bidii. Mwaka 2009, wakati huo ndiyo mitandao ya kijamii inaibuka nikajiunga na mtandao wa Facebook. Pia wakati huo Simujanja zilikuwa chache sana nikawa naenda Internet Café (Pale Magomeni, Sea Boys, ilipokuwa ofisi ya Ras Simba) na kuanza kuandika na kupost simulizi zangu za; Msafiri, Taxi ya Kijivu, My Strange Friend (ya lugha Kiingereza), Mateka n.k. Ila, kwakuwa napost simulizi huku nikiambatanisha na jalada (ambalo niliDesign mwenyewe) hivyo waandishi wengine nao kumbe walikuwa wakinifuatilia. Baadaye wakaanza kujitokeza kwa wingi wakinipa niwaundie majalada kwa ajili ya kazi zao. Hivyo nikajikuta muda wangu mwingi (wa ziada, ambao ningetakiwa kufanya kazi zangu binafsi za uandishi nikajikuta nautumia katika kuunda majalada ya kazi za waandishi), nikajikuta sipati muda wa kuandika tena seriously kwa manufaa yangu binafsi, ila kwa upande mwingine si kwamba nilipoteza ndoto/azma yangu ya tangu udogoni, ya kuwa maktaba katika vitabu, hasha! Ilitimia. Kwasababu licha ya kwamba sikuchapa kitabu changu binafsi, lakini jina na chapa yangu imeendelea kuwepo maktaba katika vitabu vingi vya waandishi wa Sasa.

**Hebu tueleze, hii graphics, unaifanya tu kwa utundu au ulisomea shuleni?**

Mwanzoni kabisa nilikuwa nafanya Fine Art yaani uchoraji wa kawaida kwa kutumia kalamu, brashi na rangi za aina aina. Sasa mwaka 2006 nikiwa kidato cha 2, Kuna brother mmoja aligundua kipaji changu, yeye ni Professional Graphic Designer mpaka leo anaendelea...hivyo ananiambia kuwa nikijifunza Graphic Desiging nitakuja kuwa 'noma' sana, maana dunia inaenda mbio sana, tunaingia kwenye teknolojia na uchoraji wa mikono hautakuwa na shughuli nyingi. Nikakubali wazo lake hivyo ikawa kila siku nikitoka shuleni siendi tena tuition pale Mchikichini (tunapaitaga Mchiki Down, Waliosoma shule za Dar' lile chimbo siyo geni kwao) Kwangu nilikuwa na wakati mgumu sana, Yaani nijifunze Graphic Designing na kujifunza kuitumia kompyuta kwa wakati mmoja....ila nilikaza. Naye alinifundisha kwa bidii na upendo kuanzia A mpaka Z, na nilipokuwa nimeiva akaniajiri kwenye ofisi yake ya Printing pale Kariakoo Hebu vuta picha, unaajiriwa na mwalimu wako!

Na katika hili pia kwa upande fulani ilinipa tena wakati mgumu, kwani ilinitaka nilinganishe mzani kati ya kazi na shule, maana wakati huo nimepata ajira nipo kidato cha tatu. Nikirudi katika swali husika ni kwamba baada ya kujifunza na kuielewa, siku za mbeleni nilienda Chuo kuisomea zaidi ili niwe na cheti kinachotambulika (ingawa ningeweza kutengeneza cheti feki na vikafanana kabisa , yes! Maana vyote hutengenezwa na designers), nikasoma na kozi nyinginezo za Multimedia kama Videography and Photography, Music Producing n.k



EMMANUEL MOSES KINDOLE "KINDO"

# JELOUSY

**Na: Sadari Kisesa**



**WHATSAPP: +255689828497**

"Hakumjua kabla, alimjua kwenye ujana, katika shule ya sekondari Yusuf Makamba. Hakuwahi kuwa mpenzi wake kabla, alikuwa mpenzi wake kipindi wote walipopendana kwa dhati. Wakasaidiana kwenye ushauri, walipendana sana lakini ghafla upendo wao ukaingia dosari. Baada kufeli mitihani ya kidato cha nne, walitengana. Wazazi wakawaacha na kila mmoja akaanzisha maisha yake katika mkoa wa Dar es salaam. Kila mmoja akapanga chumba na kuanza kujitegemea... Hussein tangu atengane na mpenzi wake hakubahatika tena kumweka machoni, yapata miaka kadhaa. Akamkumbuka kwa mengi. Alimkumbuka kipindi walichokuwa wakiwasiliana kwa simu, kipindi walichokuwa wakitakiana heri ya kumbukizi ya kuzaliwa. Alimkumbuka kipindi walichokuwa wakisoma pamoja wakijiandaa na mitihani ya mwisho ya kidato cha nne. Akamkumbuka kwa mengi, lakini leo yupo wapi na kumbukizi zote zipo wapi imebaki stori. Kumbukizi zote zimezizima kama Mshumaa. Kwenye macho imebaki taswira yake tu.

Akajitahidi kuvumilia hali anayopitia, ingawa kuna mwaka alisikia mpenzi wake ameolewa na mwanaume mwingine, akaumia sana. Mwanaume aliyemwoa kwakuwa ana wivu alimzuia kuwa na mazoea na wanaume wengine, alimkataza kuwa na mitandao ya kijamii. Kwasababu aliogopa kuibiwa Fatima mwanamke mwenye asili ya kiarabu. Kwa kufanya vile hakujua kama atamuumiza Hussein mwanaume aliyempenda mkewe kwa dhati. Mwanaume asiyezoea kukaa mbali na mkewe, aliyezoea kumwona na kuwasiliana na mkewe mara kwa mara. Hussein amekuwa mpweke sasa kwa sababu ya mwanamke asiyemwona tena machoni pake, alikuwa mnyonge mpaka akahisi kuumwa kwa kukosa kitu muhimu kwenye maisha yake. Kipindi kirefu kilipita bila kumtia machoni Fatima kiasi kwamba akahisi Mungu amempenda zaidi mwanamke wa ndoto zake. Ila nafsi ilikataa, ikasema *la-hasha! angekuwa ameaga dunia angesikia taarifa kutoka kwa watu wake wa karibu, kwasababu mficha maradhi kifo umuumbua.* Nafsi upande mwingine ikamwambia *mwanamke unayemkumbuka yupo mzima wa afya,* hakuwahi kumwona kwa kipindi kirefu lakini hakuacha kumwombea ili huko alipokuwepo aishi miaka mingi yenye furaha na upendo kwenye ndoa yake. Hakuchoka kumwomba Mungu alikesha akiomba siku moja akutane na Fatima. Amwambie jinsi gani bado anampenda...

Miaka saba si haba ni mingi tangu apotezane na kipenzi chake akipendacho, ni mingi sana hasa kwa wapendanao. Alishakata tamaa lakini kama miujiza, siku moja ilikuwa jioni kijua cha usoni kinakwenda kuzama akiwa kwenye kituo cha mwendokasi cha Kimara mwisho. Akikata tiketi kwenye dirisha namba nne kwenye mwendokasi ziendazo Gerezani, ilikuwa pembezoni mwake kwenye dirisha namba tano kwenye mwendokasi ziendazo Morocco. Akasikia sauti nyororo, ilikuwa ya mwanamke ikitoka kwenye kinywa chake ikisema.

"Kaka'angu naomba kata tiketi mbili nakuja kurudisha hela yako."

Hussein akageuka kutazama mwanamke aliyeongea nani, alistaajabu sana baada macho yake kugongana ana kwa ana na mwanamke ampendae. Mwanamke ambaye alikuwa mpenzi wake awali, mwanamke aliyekuwa na shauku ya kumwona.

"Fatima!..." akajikuta akimwita kwa mshangao huku akishikwa bumbuwazi kwa kuachama mdomo mwaaa!.

Fatima hakuonyesha uso wa furaha kana kwamba hakupenda kukutana na *ex* wake licha ya kutokuonana kwa miaka kadhaa, alionekana mtu mwenye hofu akatazama huku na huku mara akakimbia mbio akijaribu kutoweka kwenye kituo cha mwendokasi. Hussein akaacha kuchukua tiketi, alikimbia mbio akimfuata Fatima huku kichwani mwake akiwa na maswali lukuki. Akajiuliza kwanini anakimbiwa, inamaana licha ya kutokuonana kwa muda mrefu hajafurahi.

Alisema *Fatima ndiye mtu atakayejibu maswali yangu,* alistaajabu sana kumwona kweli Fatima ana lengo la kutimiza dhamira yake ya kutotaka kuonana na yeye. Akamwona kwa mbali akimaliza daraja la Kimara mwisho akishuka, alikwenda kwenye kituo cha daladala ziendazo Mbezi mwisho akapanda daladala akatokomea kwenye macho ya Hussein. Hussein akaachwa mtu mwenye msongo wa mawazo, alijiuliza maswali mengi sana. Kwanini Fatima amemkimbia, inamaana ananichukia. Inawezekana vipi watu wasionana kwa kipindi kirefu wasilakiane. Kwanini Fatima anamwogopa kama uko-

ma. Akahuzunika sana ikafika hatua almanusura adondoshe machozi mbele ya umati. Safari yake akaona chungu kinyonge akashuka katika daraja. Akavuka ng'ambo ya pili ya barabara kuu, alikatisha vichochoro kadhaa vya Kimara mwisho mara akawasili kwenye chumba alichopanga palepale Kimara mwisho mtaa wa Kinzudi.

Akafungua mlango akaingia ndani alikwenda kujibwaga kitandani chali kisha akaanza kufikiri mambo ya kutwa nzima, alizama kimawazo. Hakukumbuka hata kama hakufunga mlango. Ilikuwa ishaingia usiku alivyojilaza akapitiwa na usingizi, alichapa usingizi bila kushtuka kama hajafunga mlango wala hakula msosi wa usiku. Jogoo aliyepiga wiko mara mbili mfululizo akamwamsha, alikurupuka asubuhi ile kutoka kitandani. Polepole alikwenda msalani kujisafisha uso. Baada ya kujiandaa akaingia mtaani kwaajili ya kazi yake ya kuuza nguzo za kike za Mitumba.

“Mbona njaa imeanza mapema... Kumbe! sikula jana, nitakapokutana na mgahawa popote nitakwenda kufungua kinywa,” Hussein alisema mara baada alipokuwa njiani, alipokata mitaa huku akionyesha bidhaa zake kwa wateja. Mara akajikuta amewasili kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Kibanda cha mkaa, alishindwa kuzuia njaa kwa muda mrefu akawa akitafuta mgahawa uliopo jirani yake. Alipotupa jicho ng'ambo ya pili akaona mgahawa, umechangamka kidogo. Watu wamefurika kwenye mgahawa ule. Alijenga tabasamu si kwasababu amebahatika kuona mgahawa hapana bali amependezwa nao. Kwa haraka akavuka ng'ambo ya pili akaongoza moja kwa moja mpaka kwenye mgahawa. Alipowasili furaha ikazidi maradufu ikajionyesha dhahiri shahiri baada kuingia kwenye mgahawa na kumkuta Mama'ntilie mtu muhimu katika maisha yake, alikuwa sio mwingine Fatima. Alifubaa sura asili yake ya kiarabu ilipotea, alikonda kama Moja mpaka umbo namba nane limepotea na ziwa lilimshuka. *Bila shaka mama aliyenyonyesha au anayenyonyesha,* akawaza. Ziwa saa sita lote limepotea, alimwonea huruma sana. Fatima kwa aibu aliyokuwa nayo akataka kukimbia safari hii akadakwa mkono wa kuume, ilibidi awe mpole hakuwa na jinsi kinyonge wakaongozana na Hussein mpaka kwenye viti vitatu visivyokuwa na watu wakakaa.

“Fatima... habari ya siku nyingi?...” Hussein alihoji huku akiimarisha tabasamu kinywani, maana furaha ilioje kuonana na mwanamke umpendae na mliopotezana kwa kipindi cha miaka mingi.

“Salama...” Fatima alijibu kwa nukta, akanyamaza kidogo mara akawa mnyonge na kuonyesha dalili za kutotaka kuzungumza mengi na Hussein.
“Ama hakika leo siku ya bahati kwangu.”

“Kwanini?.”

“Kwasababu ya kuonana na mwanamke nimpendae baada kupotezana takribani miaka saba inafika, sijui...”

“Mimi sio mwanamke unipendae.”

“Unamaanisha nini?.”

“Namaanisha wewe sio mwanaume nikupendae, kwasasa nina mwanaume nimpendae. Ananipenda nampenda sana, sihitaji kusaliti...” Fatima aliongea kisha akaonyesha kidole alichovishwa pete akiashiria anachoongea anamaanisha.

“Unafuraha na ndoa yako?...”

“Ninafuraha sana na ndoa yangu...sio ndoa tu hata maisha yangu.”

“Fatima unaongopa sema kweli...mwenye furaha siku zote hawagi hivyo.”

“Nahisi tushaongea vya kutosha...kwasasa sema kilichokuleta.”

“Kurudisha penzi langu la awali.”

“Sihitaji...nishapona jeraha langu, mimi kukupenda wewe ilikuwa sababu. Wewe wa kunifedhehesha mimi...ulisema mimi mwanamke ukatamka wanawake kama sisi tunapenda pesa, kweli... Hapana, umenikosea sana na umenifedhehesha sana mbele ya umati, kwasababu wivu?... kamwe! sitoweza kusamehe. Naomba kwasasa kila mmoja achukue hamsini zake, mimi nishachukua za kwangu na kwasasa nishakuwa mke wa mtu na mama wa familia...siwezi tena kuwa na mwanaume mwingine asiyekuwa na msimamo na mwenye wivu.”

*Inaendelea Ukurasa wa 25*

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—12

MTUNZI: ASHA SIRAJ
Whatsapp 0789044345



UTANGULIZI

Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila

***Ilipoishia…***

**Ilifika muda akawa ananiambia mimi nitaendelea kuwa mfanya kazi ndani ya nyumba hiyo, nashukuru hakuwahi kunizuia nisiende chuo, yote alikuwa anafanya ila kwenye swala la ada alilipa vyema.**
**Yani sikuwa namuelewa kabisa kwanini ananaifanyia mambo kama haya, kama nimakosa yalikuwa ya kwake mwenye sasa kwanini ananiadhibu mimi.**

*Endelea…*

Nilizidi kuchoka akili kabisa nilijiona ni mtu nisiye na thamani yoyote ile ndani ya jengo hilo. Nilikuwa kama mfanyakazi wa ndani, maana niliwapikia na kuwapelekea chakula chumbani kwao.
Na baada ya kumaliza kula waliniita kuja kutoa vyombo yaani daaah mwenzenu nilichoshwa sana na tabia hizo.
Siku moja nikiwa *busy* jikoni nikiweka sawa mambo yangu ili nianze kuandaa chakula cha usiku, mara mdada huyu ambaye hata jina lake sikuwa nalijua, vyovyote vile kwanza hata ningelijua lisingeweza kunisaidia chochote kile zaidi ya kunipa maumivu tu, aliingia jikoni kwa madoido kama yote. “Nipishe jikoni mimi nimuandalie *babe* wangu chakula maana wewe umeshindwa, amemiss sana tambi hivyo naomba unipishe nimpikie mume wangu tambi”
.
Yani nilitamani nimpike yeye kwa hasira nilisonya kisha nikaondoka zangu na kuelekea chumbani. Nikatamani kulia ila nilipotezea ili maisha mengine yaendelee kikubwa nisinyimwe kula tu.
Baada ya saa moja kupita nilikuja kuitwa nikatoe vyombo, Mungu wangu nilichokumbana nacho kwenye bakuli kilikuwa kichekesho kitupu.
Tambi zilikuwa zinaelea kwenye maji kama supu ya makongoro, sijui zilikuwa zinaogelea, “hahaaaaa”, nilicheka sana hiyo siku kwa zile mbwembwe zote alizokuja nazo mapishi ndio haya.

Mara gafla nikiwa nacheka huku nakohoa vibaya, aliingia Shahdu jikoni akanikuta nikiwa nacheka ile mbaya akafunga mlango wa jikoni. Alinisogelea mpaka sehemu nilipokuwa nimesimama akanishika na kunitizama usoni kwa macho legevu yaliyojaa huruma, “Shazma ni kwamba bado unanipenda?”
Swali lake liliniacha mdomo wazi maana hizi tambi ndo zimemfanya aniulize hivo.

Nilivyopiga jicho na kuziangalia zile tambi zilivyokuwa zinaogelea nilijikuta nashindwa kujizuia nilicheka sana.
“Shazma nahitaji msamaha wako, mimi bado nakupenda, wewe ni mwanamke unayefaa kuwa ndani na wala sio Yule!”
Mmhh leo hii ndo unaniona

wa muhimu kwenye nyumba yako wakati uliniona kama kinyago na kunifanya kama msichana wa ndani kwa sababu sina pa kuishi.
Ila haya yote nimevumilia. Wakati naendelea kuongea alinishika kwa nguvu na kunipiga denda la kushtukiza.
Nilijikuta nasahau kama nina hasira naye tulinyonyana pale jikoni hadi nikajikuta namsogeza karibu yangu zaidi. Alioniomba msamaha huku machozi yakimtoka akidai ni kweli amefanya makosa mengi kwangu.

Ukweli nilikuwa nampenda sana Shahdu pamoja na yote aliyonifanyia ila moyo wangu bado ulikuwa unapenda.
Aliniambia ananipenda, zaidi ya mara hamsini alirudia neno nakupenda kila wakati. Nilimjibu “kweli kama unanipenda basi naomba ukamfukuze yule mwanamke ndani ya hii nyumba.
Alikubali na kuniambia “nipo tayari kumfukuza humu ndani ila sipo tayari kukupoteza wewe shazma”.

Nikweli alifungua mlango wa jikoni akielekea chumbani alipo kishikwambi yule mimi nilikuwa nikifuatia kwa nyuma huku nikiwa nachekelea tu.
Weee kiliumana mle chumbani Shahdu alikusanya kila kitu chake na kuvitupa nje alimtimua ndani mimi nikabaki kucheka tu, huku nikimwambia “uwe unakoma kuingilia mapenzi ya watu”.

Yani kama kuna wanawake wa hivi nawaambia acheni hizo tabia hujui mwenzio amepitia mambo mangapi mpaka kuwa na *boyfriend* wako alafu wewe unatokea huku unaingilia kati.
Mambo ya kuingilia mapenzi ya watu sio vizuri unaingia kwa majivuno mwisho unafukuzwa kama paka aliyekodolea samaki, ni aibu jamani wanawake wenzangu tujifunzeni basi hata kwenye hii hadithi maana daah!
Asilimia nyingine wanawake mna hizi tabia kisa fulani amegombana na mpenzi wake hujui shida nini wewe huyu unakimbizia vironjo vyako eti ukamharibie zaidi, hayo sio maisha.

Baada ya yule mwanamke kuondoka mapenzi yangu mimi na Shahdu yalizidi kupamba moto na miezi ilisogea na mapenzi yetu yalizidi kuwa moto.
Tokea hapo Shahdu hakuwahi kufanya ujinga huo tena, michakato ya mimi na Shahdu ya kufunga ndoa ilianza baada ya mwezi mmoja tulioana na kuishi kama wanandoa. Kwa iufupi maisha yetu yalikuwa matamu na ya kuigwa na kila mtu. Tulijaaliwa kupata mtoto wa kiume, maisha yetu yalikuwa pambe.

- MWISHO. -

**SHUKRANI**

JARIDA la Ngurumo ya Mwandishi tunamshukuru sana Mwandishi ASHA SIRAJ kwa kukubali kutupatia hadithi yake hii ili kuchapwa hapa jaridani kwa minajiri ya kuburudisha wasomaji



**KISIWA CHA UOKOZI**

*Inaendelea ............*

Siku moja niligundua kuwa kuna kisiwa jirani ambapo kunasikika sauti za furaha kila siku. Nilipouliza nikajibiwa kuwa ni kisiwa jirani huwa wannafanya sherehe kila wanaporudi kutoka kutafuta lulu. Hicho ni kisiwa pekee kinachofahamika kwa kuwa ni wafanyabiashara wa lulu. Basi kwa kuwa sikuijua lulu ilibidi niumuombe ruhusa mfalme ili na mimi nikashuhudie sherehe zao na nipate kuijua lulu. Mfalme alikubali na akanipa msafara wa wafanyakazi wake waende pamoja nami.

Tulipofika kule nilifurahi kuiona lulu kwa mara ya kwanza na nikafurahia pia sherehe zao. Basi katika hali kama zile nilishangaa kuona kuwa watu wanashusha mizigo kutoka bandarini lakini katika ile mizigo kuna ambayo imeandikwa Sinbad, nilipoangalia kwa uzuri nikagundua kuwa nahodha wa lile jahazi alikuwa ni yule nahodha wetu. Hivyo kumbe zile mali zilikuwa ni zakwangu na lile jahazi lilikuwa ni lile letu. Nikamuita kijana mmoja na nikamuuliza habari zao na akanieleza kuwa walibahatika kuliokoa jahazi lao na watu wote walipona isipokuwa Sinbad ndo hakuonekana. Kijana huyu alizungumza bila ya kunijuwa kama ndo mimi

Basi nikamfuata nahonda na kumueleza kuwa mimi ndo Sinbad na zile mali ni za kwangu. Basi nahonda aliponiona akanikumbuka na kutoa machozi kwa furaha maana walifahamu kuwa nimekufa. Nahodha akanikabidhi mali zangu na nikaziuza, nikapata habari kuwa jahazi letu litarudi Baghdad wiki ijayo. Nilichukua bidhaa zangu na kuuza baadhi na kurudi kwa mfalme na baadhi ya bidhaa. Nikamuelezea kilichotokea na alifurahi sana kwa kupata bidhaa zangu. Na hivi ndo Mwenyezi Mungu anavyowafanyia watu wenye subira.

Nikampatia mfalme bidhaa zilizobaki kama zawadi na nikamuomba ruhusa ya mimi kurudi nyumbani kwetu wiki ijayo. Kwa majonzi na kinyongo mfalme aliniruhusu na hata binti yake alikuwa na majonzi sana lakini haina budi "milima haikutani binadamu hukutana" ni maneno nilojisemea moyoni. Basi wiki ilipoisha mfalme alinipatia mali nyingi sana kama zawadi. Nilipata pia lulu kutoka kwenye kisiwa kile. Kwa hakika katika safari hii nilipata taabu na faida kubwasana.

Tulipofuka Baghdadi niliwaelezea ndugu zangu habari ya yalonikuta, kwakweli waliniambia niwachanena habari za biashara hii. Hata mimi nikajiapiza kwa yalonikuta kwa hakika sitarudia tena bishara hii. Basi nikatoa sadaka kutoka katika faida yangu na nikatoa na zaka muda ulipo fika. Nilitumia faida ile kujiendeleza kibiashara hata miezi mingi ikapiata. Nilisahau kabisa yalonikuta kwenye safari ile. Baada ya muda nahodha wetu wa mwanzo nilikutana nae, na katika mazungumzo yetu alinieleza kuwa wanatarajia kuanza safari wiki ijayo. Kwa hakika nilivutiwa tena na biashara ile. Na kwa kuwa nilisahau machungu yalonikuta katika safari ya kwanza nikaazimia kuanza safari ya pili wiki ijayo. Mpaka kufikia hapa Sinbad kwa baharini akamaliza kusimulia hadithiya safari yake ya kwanza. Na kwa kuwa muda ulukuwa umekwenda hakuweza kuanza hadithi ya safari yake ya pili. Basi akampatia Sinbad mbeba mizigo zawadi nyingi na pesa kadhaa ya kutumia kama fidia ya kuvunja kazi zake. Na akamuahidi kesho awahi kuja maana safari ya pili ina mambo mengi na makubwa zaidi kuliko ya kwanza.

**SAFARI YA PILI YA SINBAD**

Basi siku ile Sinbad mbeba mizigo aliwahi haraka sana na mapema zaidi, na akamkuta Sinbad wa baharini ameshakaa na watu wake wanamsubiri kuanza hadithi. Walipokusanyika watu wote vikaagizwa vinywaji na vileja na kuanza kula huku wakisikiliza hadithi. Sinbad wa baharini akaanza kusema "basi tambueni kuwa sfari hii ya pili nilikutwa na makubwa zaidi kuliko hii ya kwanza. Ha ilikuwa hivi:-

Basi tulipozungumza na nahodha kuwa wiki ijayo wataanza safari nilirudi nyumbani na kujiandaa kwa safari. Ndugu zangu walijaribu kunizuia lakini sikuwasikia "sikio la kufa halisikii dawa" wengine wakanambia najipeleka nikafe ila sikuwasikiliza. Maandalizi yalikamilika kwa siku mbili na nikawa nasubiria safari tu. Wiki ilipofika tukaanza safari kwa amani lakini siku ya tatu kabla ya kuingia kisiwa cha kwanza kufanya biashara hali ya hewe ikabadiliki ghafla.

*Itaendelea toleo lijalo*

**Je unafurahishwa na jarida letu?**

**Tuambie kupitia Whatsapp**


**+255 766 974 865**

# VITABU VYA WASHINDI WA TUZO NYERERE VYAZINDULIWA

KAMATI ya Tuzo ya Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania chini ya Wizara ya Elimu imezindua vitabu vya washindi wa Tuzo hiyo msimu wa pili.

Hafla hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Kijitonyama Mwezi wa Februari mwaka huu ilihudhuriwa na wageni mbalimbali: waandishi bunifu na wadau wa fasihi Tanzania.

Hii ni moja ya ahadi iliyowekwa na kamati hiyo kwa kila mshindi wa kwanza katika Riwaya, Ushairi, Tamthiliya na Hadithi za watoto. Kati ya vitabu hivyo vilivyochapishwa ni pamoja na Riwaya mpya ya Garasa cha Laura Pettie, hadithi za watoto cha Tune Shaaban Salim Maziwa ya Kuku na diwani yake Mohamed Omar Juma Ngoma ya Muwele.




Aidha Mwenyekiti wa tuzo hiyo Prof. Penina Mlama alitoa wito kwa waandishi kuendelea kujitokeza kuwasilisha miswada yao pindi muda utapotangazwa kwani tuzo hiyo hutolewa kila mwaka.

Naye aliyekuwa mgeni rasmi Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (MB) aliipongeza TET kwa kuendelea kutekeleza shindano la tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, amesema kuwa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi bunifu ni nyenzo muhimu ya kuibua na kukuza vipaji vya waandishi wa ndani. Pia aliongeza kusema kwamba tuzo hiyo, ameeleza kuwa mpango huo ni chombo cha kitaifa cha kutambua ubunifu na kuendeleza utaamaduni wa Kiswahili kupitia maandiko ya waandishi chipukizi na waliobobea.

Utoaji tuzo kwa washindi  wa msimu wa nne utafanyika tarehe 13 April, 2026 jijini Dar es saalam katika ukumbi wa Super Dome, Masaki.

**Prof. PENINA MLAMA**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo Nyerere ya Uandishi Bunifu**



## Nyota ya Mashariki Umm Kulthum…
## Sauti iliyowaunganisha Waarabu

**Na: Mervat Sakr**

Taifa la Kiarabu halikuwahi katika historia yake ya kisasa kuijua sauti ambayo mioyo iliizunguka na kuikumbatia kama ilivyoizunguka sauti ya Umm Kulthum. Hakuwa tu mwimbaji, wala hakuwa tu tukio la kisanii; alikuwa dhamiri ya taifa zima, na sauti ya kipindi kirefu cha historia yake. Katika koo lake zilikusanyika matumaini ya watu na maumivu yao, ushindi wao na huzuni zao, furaha zao na nyakati zao za dhiki. Ndiyo maana haikuwa ajabu kuitwa "Nyota ya Mashariki" na "Bibi wa Uimbaji wa Kiarabu", na kubaki hadi leo kuwa alama ya kisanii na kibinadamu ambayo ni vigumu kurudiwa.

Amezaliwa Fatima Ibrahim Al-Sayyid Al-Baltaji tarehe Mei 4, 1898 katika kijiji cha Tamay Al-Zahayira, wilaya ya Al-Sanbalawain, mkoa wa Dakahlia. Alikulia katika familia ya hali ya kawaida; baba yake alikuwa muadhini wa kijiji na pia mwimbaji wa kaswida za kidini. Hivyo alikulia katika mazingira ya usomaji wa Qur'ani na uimbaji wa dini. Tangu utotoni alivutia kwa uzuri na nguvu ya sauti yake; alikuwa akirudia nyimbo za kidini nyuma ya baba yake na kaka yake, kabla ya kupanda jukwaani kuimba mbele ya hadhira akiwa bado mdogo, akizunguka vijiji na miji ya Misri.



Mwanzoni mwa miaka ya ishirini alihamia Kairo, na hapo safari yake kubwa ikaanza. Alikutana na wanamuziki na washairi wakubwa, akiwemo Sheikh Abu Al-Ala Muhammad, kisha mshairi Ahmad Rami aliyemkuzia upeo wa lugha na mashairi ya Kiarabu, jambo lililomfanya akomae zaidi na kupaa kisanaa. Kwa kuanza kwa matangazo ya Redio ya Misri mnamo mwaka 1934, sauti yake ikawa mgeni wa kila mwezi anayesubiriwa na mamilioni katika Alhamisi ya kwanza ya kila mwezi, hadi hafla zake zikawa desturi ya Kiarabu iliyowaunganisha watu; mitaa ilisimama, na mikahawa pamoja na nyumba zilisikiliza kutoka Bahari ya Atlantiki hadi Ghuba ya Uarabuni.

Umm Kulthum aliimba takribani nyimbo mia saba, na alishirikiana na watunzi wakubwa wa enzi yake kama Abu Al-Ala Muhammad, Zakaria Ahmad, Riyad Al-Sunbati, Muhammad Al-Qasabji, Muhammad Abdel Wahab, Muhammad Al-Mougi, Baligh Hamdi na Kamal Al-Tawil, miongoni mwa wengine. Alikuwa makini katika kuchagua maneno na mizani ya muziki, akipendelea fasaha ya Kiarabu sanifu na hadhi ya kaswida. Aliimba mashairi ya Ahmad Shawqi, Ahmad Rami, Hafez Ibrahim, Ibrahim Nagi na washairi wengine wakubwa, hivyo uimbaji ukapaa hadi daraja la ushairi, na ushairi ukapaa kupitia sauti yake hadi upeo wa kudumu.

Sanaa yake haikuwa mbali na masuala ya taifa lake na umma wake; aliitumikisha sauti yake kwa ajili ya Misri na ulimwengu wa Kiarabu, akaimba kwa ajili ya taifa katika nyakati za ushindi na majonzi, na akazuru miji mikuu ya Kiarabu na Ulaya katika matamasha ambayo mapato yake yalielekezwa kusaidia juhudi za kitaifa. Alikuwa balozi wa sanaa ya Kiarabu, akibeba ujumbe wake kwa heshima na hadhi, akihifadhi taswira yenye staha ya msanii mwanamke, aliyekusanya baina ya utulivu wa heshima na nguvu, baina ya haiba na unyenyekevu.

Hakuishia katika uimbaji na matamasha pekee; aliingia pia katika ulimwengu wa sinema na akatoa filamu sita, ya kwanza ikiwa "Widad" mwaka 1936, na baadaye kazi nyingine hadi filamu "Fatima" iliyokuwa kuonekana kwake kwa mwisho kwenye skrini. Katika kila tajriba, alikuwa akiongeza ukurasa mpya katika hazina yake ya kisanii na kuimarisha uwepo wake katika dhamiri ya Kiarabu. Umm Kulthum alipata heshima nyingi; alipewa pasipoti ya kidiplomasia kwa kutambua mchango wake, na akatunukiwa nishani nyingi kutoka nchi za Kiarabu na za kigeni. Hata hivyo, nishani kuu aliyobeba haikuwa ya chuma inayoning'inizwa kifuani, bali ilikuwa mapenzi ya umma yaliyomzunguka katika maisha yake na hata baada ya kuondoka kwake.

# KITABU NILICHOSOMA


## MY LIFE, MY PURPOSE – 04

UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA

"MY LIFE, MY PURPOSE"

Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA

{Imetolewa kutoka mtandaoni}




Inaendelea…

4. URAIS

Baada ya kutafakari na kushauriana na rafiki zake, Mheshimiwa Mkapa kwanza alimwambia mama Anna juu ya kugombea Urais. Mama Anna alisita kidogo ila akakubali. Pili alimueleza Mwalimu kwa barua kwani alikuwa Butiama, kisha akukutana nae ana kwa ana. Alimpa mwalimu sababu kuu nne za uamuzi wake wa kutaka kugombea.

Kwanza alitaka kurekebisha na kurejesha uhusiano chanya kati ya chama na serikali yake, na vyama vya ushirika ambao ulikuwa umefifia. Pili, alitaka kuhimarisha uhusiano na vyama vya wafanyakazi ambao walikuwa wanatishia kugoma kwa mara ya kwanza. Tatu, ilikuwa kurekebisha mahusiano mabaya na wahisani kuhusiana na kushamiri kwa rushwa. Nne, alitaka kurudisha uhusiano na mashirika ya fedha ya kimataifa ambao walikuwa wamekataa kuanzisha miradi mipya.Mwisho aliwapima hao waliokuwa wamechukua fomu akaona atajilaumu hapo baadae kama naye hata gombea.

Mwalimu alimshukuru, akamwambia hakuwaza kuwa nae angegombea, alikuwa anamfikiria mtu mwingine ambaye alikuwa anasita sita. Akamwambia hatamzuia kama amefanya uamuzi huo. Mwalimu aliwaomba watu kadhaa kumuunga mkono, Mwalimu alipenda hasa uwezo wake wa kufanya maamuzi, Mwalimu alishiriki katika kampeni ambapo Mheshimiwa Mkapa alisisitiza ilani, sio mambo binafsi. Mdahalo wa wagombea wote ambao ulirushwa mubashara ndio ulimfundisha njia ya ushindi. Ulikuwa "Game Changer" anasema.

November 23, 1995 aliapishwa kuwa Rais. Katika kuunda Baraza la Mawaziri, Mwalimu alikataa kujihusisha hakuwa muingiliaji – interventionist. Mheshimiwa hakuwa mgombea wa mtu kwa hivyo hakuna aliyetegemea fadhila.

Hali ya nchi ya uchumi ilikuwa mbaya sana lakini anasema sikuogopa, kiongozi lazima awe jasiri. Alikumbana na uzembe, kutowajibika na rushwa.

Kazi kubwa - kwanza ilikuwa kuwashawishi wahisani kuwa mambo yatabadilika. Nchi ilikuwa na madeni makubwa sana. Deni letu lilikuwa dola bilioni saba, tulisamehewa bilioni tatu, hii ilikuwa hatua kubwa sana na ilimfurahisha Mwalimu ambaye alishaanza kuumwa.

Mheshimiwa aliamini tulihitaji kujiangalia upya na kujifikiria kimkakati upya namna tulivyo kuwa tunaendesha nchi.

Mheshimiwa anasema kuwa walio iona staili yake ya "Kusema na kuelekeza" kuwa ilijaa kiburi na majivuno ilikuwa lazima kuonyesha kuwa hata tetereka.

Matokeo yake ni kwamba mapato yaliongezeka karibu mara tatu kutoka dola 612,587 mwaka 1995 kufikia dola 1,796,862 miaka kumi baadae. Fedha za kigeni ziliongezeka kutoka uwezo wa kununua bidhaa za mwezi mmoja na nusu kufikia uwezo wa kununua bidhaa za miezi mitano na theluthi moja. Riba za benki ilishuka kutoka asilimia 36% kufikia asilimia 15% mwaka 2005.

Ilianzishwa TRA kuimarisha ukusanyaji wa mapato Julai 1996.Ukaanzishwa mfumo wa VAT Julai 1998Public Service and Act pamoja na Public Procurement Regulatory Authority vilianzishwa 2001Commision for Human Rights and Good Governance ilianzishwa Julai 2001Prevention of Corruption Bureau nayo ilianzishwa, Mheshimiwa akaitwa Mr cleanRegulatory Agencies nyingine zilianzishwa nyingi ikiwa ni pamoja na Brela, EWURA, TCCRA,SUMATRA, Viwanja vya ndege,Maji safi na taka, TANROADS,na National Business Council kuhimarisha mahusiano na wafanya biashara.

Kati ya mageuzi tuliyofanya yaliyokuwa na utata sana ni kubinafsisha mashirika ya Umma, mageuzi/maboresho ya utumishi, na uuzaji wa nyumba za Serikali.

*Inaendelea*

# HABARI PICHA


## Uzinduzi wa Vitabu vyaWashindi wa Tuzo Nyerere Msimuwa Pili




Kikundi cha ngoma kilichotumbuiza siku ya uzinduzi wa vitabu vya washindi wa Tuzo Nyerere Msimu wa pili



Wanafunzi wa shule za msingi walikuwa ni miongoni mwa wageni wa siku hiyo,.




Pichani ni Mwandishi wa kitabu cha GARASA Laura Pettie (kushro) akiwa na Dkt. Aneth Komba Mkurugenzi wa TET




Mwandishi Tune Shaaban akikabidhi vitabu vya kuzinduliwa kwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia



**Pichani, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mh. Prof.** Adolf Mkenda (mwenye suti) akiingia katika eneo la tukio



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia akitazama ubora uliotumika katika uchapaji wa moja ya vitabu vilivyozinduliwa

## MAMA YANGU

Ulinizaa kwa tabu, maumivu na uchungu
Kunileta duniani yote mapenzi ya Mungu
Mbona wawa mkali kama mwibawe Nungu-nungu

Muungwana akikosa shuti yeye kuchutama
Mwanadamu mwenye ponyo si mwingine bali mama
Kama nahodha shusha tanga pepo zim-echachama

Ni imani ya wa kale kuwa mkulungwa hakosei
Maisha si yaleyale kama mbio za Koskei
Lisemwalo sikia, hata ushauri hupokei?

Mabanati huwaonao hujifunza kwa zako nyendo
Jeuri, kukunja sura ndo waige huo mtindo?
Wajua majibuyo hutupa findofindo
Kuwa makini mzazi maana ndoo hujazwa kwa ndondondo

Tuliza nyumba itulie
Ukiondoka tukulilie
Majuto usitutie
Bali mazuri tutarajie

Chochea kuni za wema
Moto wa upendo uwake hima
Ulionalo jiko ni lako mama
Usiogope kuweka kuni za kima

Stawisha nyumbayo
Majirani watamani yo
Na wala usiwe mchoyo
Sikia watu wayasemayo

Usinifanye mwanao nijilaumu kwanini umenizaa?

# TAHARIRI

## AMANI NI TUNU

Wapendwa,

Amani katika maisha tuliyo nayo si jambo la ku-chezea hata kidogo. Siku zahivi karibuni limeibuka wimbi kubwa lakushabikia vita vinavyoendelea huko Mashariki ya kati.

Tumewahi kujiuliza maumivu wanayoyapata wana-damu wenzetu kule Mashariki ya kati? Tumewahi kujiuliza maisha yao yatakuwaje baada ya hapo?

Vita si jambo la kushabikia wala si jambo la kupend-wa. Ni jambo baya ambalo kwalo watoto hubaki yatima, miji hubaki ukiwa, mioyo hubaki na visasi visivyo na mwisho, uoendowa mtu na mtu hupun-guana kadharika.

Je huo ndiyo mpango wa Mungu katika maisha ya mwanadamu?

Tumshukuru Mungu kwa kuwa nchi yetu haipo kwenye machafuko kama hayo, lakini kile tu tuli-chokionja kwa saa 72 mpaka sasa kimeacha mpasu-ko kati yetu, watu hawajali utu wa mwingine, roho za visasi zimegandamana na dhamira zetu.

Haya ni madhara ambayo kufutika kwake katika moyo wa mwanadamu huchukua karne nyingi.

Tuungane pamoja, tusali na kuomba amani kila mtu kwa imani yake. Ili dunia iwe pahala pema pa kuishi ambapo kila mmoja wetu atafurahia uzuri waumbaji wa Mungu ndani ya huyu Mama Duania.

Wakatabahu!

*R.R. Mwambe*
Iringa —Tanzania

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu: 0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
15,000/= tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# KUTOKA MAKTABA
# ELVIS ESTABULUS MUSIBA

Elvis Musiba (1950–2010) alikuwa mmoja wa waandishi maarufu na wenye ushawishi mkubwa nchini Tanzania, hususan katika aina ya riwaya za kijasusi na kusisimua (thrillers).

**Mambo yanayofanya akumbukwe**

**Mhusika Maarufu:** Willy Gamba Musiba anajulikana zaidi kwa kumuumba mhusika Willy Gamba, jasusi shujaa wa Kitanzania ambaye mara nyingi alikuwa akipambana na maadui wa ndani na nje ya nchi ili kulinda maslahi ya taifa na bara la Afrika. Willy Gamba alikuwa kama "James Bond" wa Afrika Mashariki.

**Kazi Zake Maarufu**

Aliandika riwaya nyingi ambazo zilipata wasomaji wengi sana kutokana na lugha yake rahisi ya Kiswahili na visa vya kusisimua. Baadhi ya vitabu vyake ni:

Njama
Kufa na Kupona
Hofu
Kikosi cha Kisasi
Jiko la Sumu

**3. Mchango Wake Kitaaluma na Kijamii**

Mbali na uandishi, Musiba alikuwa mfanyabiashara na kiongozi katika tasnia ya habari na biashara: Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAJA). Alihudumu kama Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA). Alikuwa mshauri na mdau mkubwa katika kukuza matumizi ya Kiswahili fasaha kupitia fasihi simulizi na andishi. Kazi zake zilisaidia sana kukuza utamaduni wa kusoma nchini Tanzania katika miaka ya 1980 na 1990, na hadi leo vitabu vyake bado vinatafutwa na wapenzi wa riwaya za kijasusi.

**Historia ya maisha yake**

Aristablus Elvis Musiba (maarufu kama A.E. Musiba) ana historia ya kipekee kwani aliishi maisha yenye nyanja mbili kuu: uandishi wa fasihi na uongozi wa kibiashara nchini Tanzania.

**Maisha ya Awali na Elimu**

Elvis Musiba alizaliwa mnamo 1950 *(baadhi ya vyanzo vinataja mkoa wa Mara).* Alikua katika kipindi ambacho Tanzania *(wakati huo Tanganyika)* ilikuwa ikielekea kupata uhuru na



kuanza kujenga utambulisho wake. Elimu yake na mazingira ya siasa za ukombozi wa Afrika viliathiri sana fikra zake, jambo ambalo lilionekana baadaye katika maandiko yake.

**Gwiji wa Riwaya za Kijasusi**

Musiba alianza kupata umaarufu mkubwa katika miaka ya 1970 na 1980. Alikuwa mmoja wa waandishi wa kwanza nchini Tanzania kuandika riwaya za kusisimua (thrillers) zilizokuwa na mwelekeo wa kisiasa na kiusalama.

**Willy Gamba:** Aliunda mhusika Willy Gamba, jasusi ambaye hakuwa tu mpelelezi, bali alikuwa mwanaharakati wa ukombozi wa Afrika. Mara nyingi Willy Gamba alitumwa kupambana na mamluki, majasusi wa mataifa ya nje, na mifumo ya ubaguzi wa rangi *(Apartheid)* ili kulinda usalama wa Afrika.

**Mchango:** Vitabu vyake kama Kufa na Kupona na Njama vilihamasisha uzalendo na kuifanya lugha ya Kiswahili itumike kuelezea mambo magumu ya kijasusi.

**Maisha ya Biashara na Uongozi**

Mbali na kalamu, Musiba alikuwa mwanachama mahiri wa sekta binafsi na alijitolea sana kuimarisha biashara nchini Tanzania.

**Habari:** Alikuwa mdau mkubwa wa tasnia ya habari, akihudumu kama mwenyekiti wa bodi mbalimbali na kusaidia katika ukuaji wa uhuru wa habari.

**Ushauri:** Alikuwa akitambulika kama mshauri wa masuala ya kijamii na kiuchumi, akishirikiana na serikali na mashirika ya kimataifa.

**Kifo na Urithi**

Elvis Musiba alifariki dunia mnamo Novemba 2, 2010, huko Johannesburg nchini Afrika Kusini alipokuwa akipata matibabu.

**Kurejea kwa Willy Gamba:** Baada ya kifo chake, kazi zake zilipata "uhai mpya" mnamo mwaka 2018 wakati familia yake na wachapishaji wa Mkuki na Nyota walipoamua kuchapa tena vitabu vyake ili vizazi vipya viweze kuvipata.

**Athari:** Hadi leo, anachukuliwa kuwa baba wa riwaya za kijasusi za Kiswahili. Waandishi wengi wa sasa wa aina hiyo ya vitabu nchini Tanzania wanamtaja yeye kama chanzo cha msukumo wao.

# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI—9

**KANUNI BORA ZA MALEZI**

**9.0 Utangulizi**

Malezi ni safari ya maisha ambayo huunda tabia, fikra, na hisia za mtoto. Safari hii ina kanuni nyingi, lakini kuna kanuni ambazo zinaweza kumsaidia mzazi au mlezi kumwandaa mtoto mwenye uthabiti, heshima, na uwezo wa kushughulikia changamoto katika maisha yake ya sasa na baadae. Katika sura hii, tutachunguza kanuni muhimu tano kama zilivyochambuliwa na Dr. Aliza, tukianza na mahusiano bora, ambayo ni msingi wa malezi yoyote yenye mafanikio.

Mahusiano bora husaidia mtoto kujenga msingi wa kujiamini, kuelewa hisia zake, na kushirikiana vizuri na wengine, kuanzia familia, shuleni hadi mahusiano ya kijamii.

**9.1 Mahusiano Bora**

Mahusiano ni msingi wa malezi bora. Mtoto anapokuwa na mzazi au mlezi ambaye ni thabiti, mwenye upendo, na anayesikiza, hujenga msingi wa kujiamini na kushughulikia changamoto za maisha. Mfano ni mtoto anayepata malezi mazuri na msaada kutoka kwa wazazi wake, pale anapokuwa na changamoto, mtoto hujifunza kuwa hisia zake ni halali na kuwa na ujasiri wa kujaribu tena.

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

Uhusiano mzuri hujenga imani, upendo, na heshima kati ya mzazi na mtoto, jambo linaloimarisha malezi yote mengine. Na pia inamsaidia kuwa na mahusiano bora na wengine, kwa sababu anakuwa tayari ameshajifunza kuishi kwa kutegemeana. Mahusiano haya hutoa msingi wa kisaikolojia ambapo mtoto anajua ana mtu wa kumsaidia, kumwelewa, na kumlea kimsingi, jambo linalochangia ustawi wake wa akili, kihisia, na kijamii.

**9.1.1 Faida Katika Mahusiano Mazuri katika Malezi**

Faida za mahusiano bora ni nyingi na zinaathiri malezi kwa njia ya moja kwa moja. Kwanza, mtoto hujenga ujasiri na kujiamini. Kwa mfano, mtoto anayepata mzazi wa kumtazama na kumwelewa anapokuwa na hofu ya kujaribu kitu kipya, anajua ana msaada wa kihisia na hivyo anajitahidi kushirikiana, kujaribu michezo mipya, au kushiriki mashindano shuleni bila woga au chochote kile katika maisha. Pili, mahusiano bora hutoa msaada wa kihisia wakati wa changamoto. Mtoto anapokabiliana na migongano ya marafiki au mitihani ya shule, kuwa na mzazi anayemwelewa husaidia kudhibiti msongo wa mawazo na hofu.

Kwa mfano, mzazi kumfundisha mtoto mbinu za kufikiri kabla ya kuchukua hatua, humsaidia kushughulikia hali hizo kwa busara na kwa ujasiri. Tatu, uhusiano mzuri husaidia mtoto kujenga tabia za kijamii na kujifunza kuheshimu wengine. Mfano mtoto kushirikiana na wenzake kwenye michezo ya kikundi, kujifunza kusubiri, kuzungumza kwa heshima, na kushirikiana.

Mara nyingi tabia hizi hujifunza nyumbani kutoka kwa wazazi mwenye heshima na subira.

**9.1.2 Hasara Za Kukosa Mahusiano Bora Katika Malezi**

Kukosa mahusiano ya karibu kunaweza kuathiri malezi kwa njia hasi. Mtoto ambaye hana mzazi au mlezi wa karibu mara nyingi hupata hofu ya kushindwa, ukosefu wa imani, au kujiamini kidogo. Kwa mfano, mtoto ambaye hana mtu wa kuzungumza naye anapokabiliana na changamoto shuleni anaweza kujikuta akishindwa kushirikiana na wenzake au kutojaribu kitu kipya kutokana na hofu ya kukosolewa.

Kutokuelewana au kukosa uhusiano mzuri pia kunaweza kusababisha migongano ya mara kwa mara, kwani mtoto hana mfano wa kujieleza kwa heshima au kushughulikia migongano ya kihisia. Hatimaye, mtoto anaweza kushindwa kujenga uhusiano mzuri na wengine, jambo linaloweza kuathiri maisha yake ya kijamii na uhusiano wa baadaye.

**9.1.3 Nini cha Kuzingatia Katika Mahusiano Bora**

Ili kuunda mahusiano bora, mzazi anapaswa kuwa thabiti na wa karibu, kwani mtu mmoja wa kuaminika ni bora kuliko wengi wasio thabiti. Kuonesha upendo wa kweli ni muhimu; sio tu maneno, bali vitendo vinavyoonyesha msaada, kuelewa hisia, na kushirikiana na mtoto. Kusikiliza kwa makini hisia za mtoto ni msingi wa uhusiano mzuri; mzazi anapaswa kuelewa huzuni, furaha, na wasiwasi wa mtoto na kuonyesha kuwa

# ELIMU JAMII

anathamini hisia hizo. Kwa mfano, mzazi kuzungumza na mtoto na kumuliza jinsi siku yake ilivyokuwa, kisha kumweleza njia za kushughulikia changamoto, hujenga msingi wa kuaminiana na kuonyesha upendo wa dhati.

**9.1.4 Njia za Kuimarisha Kujenga Mahusiano Bora Katika Malezi**

Njia za kuimarisha mahusiano bora ni muhimu katika malezi ya kila siku. Kutumia muda wa pamoja katika michezo, mazungumzo, au shughuli za kila siku husaidia mtoto kujua kuwa ana mtu wa kumsaidia. Pili ni kuzingatia hisia za mtoto: kuelewa huzuni, furaha, na wasiwasi ni njia ya kuonyesha upendo wa dhati. Pia, mzazi anapaswa kuwa mfano wa maadili na tabia nzuri; mtoto anapomuona mzazi akishughulikia migongano kwa heshima na subira, anajifunza kufanya vivyo hivyo katika maisha yake.

**9.1.5 Vikwazo Vinavyoweza Kuzuia Mahusiano Bora katika Malezi**

Katika hii dunia ya sasa changamoto kubwa ambayo inaweza ikazuia mahusiano bora katika malezi, ni teknolojia. Teknolojia sasa imekuwa ni kama ukuta kwa wazazi kuwasiliana na watoto wao. Mtoto akitoka shuleni anawashiwa runinga aangalie katuni, wazazi wapo na simu jannja wanaperuzi mtandaoni.

Kunakosekana muda wa kuwasiliana na Watoto, kujua maendeleo yao au kama kuna changamoto ambazo zinawakabili. Changamoto nyingine ni kufanya kazi muda wote na kukosa muda wa kukaa na familia hii pia inapelekea kuvunjika kwa mahusiano bora katika familia na hivyo kumuacha mtoto katika changamoto kubwa za kihisia na kisaikolojia.

**Hitimisho;** Mahusiano bora ni msingi wa malezi yenye mafanikio. Bila uhusiano mzuri, kanuni zingine za malezi hazitakuwa na nguvu kamili. Kwa kuwekeza kwenye mahusiano ya kupendeza na ya kuaminika, mzazi au mlezi huunda msingi wa mtoto kuwa na uthabiti, kujitegemea, na kuweza kukabiliana na changamoto za maisha ya sasa. Mahusiano haya humfundisha mtoto thamani ya heshima, subira, na upendo, jambo linalomsaidia kuwa kiongozi mwema wa baadaye katika jamii na nyumbani.

## JELOUSY

Na: Sadari Kisesa

"Ilikuwa awali kwasasa, nishatambua thamani ya mwanamke kwenye maisha yangu."

"Ushatambua thamani ya mwanamke, tafuta mwanamke mwingine wa maisha yako...mimi nishafungua ukurasa mpya wa maisha yangu, kwasasa nina mume na watoto wawili wanaonitegemea. *I am very sorry if I have offended you..."* Fatuma alisema kwa kujiamini kisha akataka kuondoka, kabla hajapiga hatua kadhaa akadakwa mkono wa kushoto. Alipogeuka akageuka na kofi zito matata alilopiga kwa mkono wake wa kuume kwenda kwa mlengwa, akasonya sonyo la *mate tulia ndani nje kuna Surua*.

"Nakuchukia, sikupendi na sitaki kukuona daima" akakazia.

"Naelewa hisia zako na nakubali kama nilifanya kosa, nakuhitaji na nahitaji msamaha wako...mimi binadamu sijakamilika unavyotamka maneno hayo inakuwa sio haki, nisamehe sana Fatima" akajishusha.

"Kama kukusamehe nishakusamehe zamani...lakini kwasasa nimeamua sihitaji kukuona na nahitaji kusahau. Ondoka."

"Naheshimu maamuzi yako, ila... Naondoka."

Hussein akaondoka kinyonge huku akijitwika mzigo wa lawama, alijiuliza kwanini nimemfananisha Fatima na wanawake wengine wapenda pesa. Baada kutambua kosa akajuta ingawa alikuwa ameshachelewa amekuta mwana sio wake tena, alipagawa sana akaona siku imekuwa mbaya kwake. Njaa ikaisha bila kupenda, aliahidi tangu siku hiyo atathamini mwanamke na hatofanya kosa kama awali.

"Mahusiano ya mapenzi yanahitaji mtu makini, mwenye kumwelewa mwenza kama anavyojielewa. Mwamini mpenzi wako, usipomwamini utahisi anakutumia. Utamwonea wivu na mara ghafla, moyo wako hutopenda. Epuka kitu wivu kwenye mahusiano, maana wivu adui namba Moja kwenye mahusiano. Wahenga usema… 'wivu kidonda ukiendekeza utakonda'".

MWISHO.

# K.O.K.W.A—2

**K.O.K.W.A**
**Mchezo mwingine mgumu mno ambao KAMANDA AMATA anakutana nao katika maisha yake ya UJASUSI.**

**Aisee hiki ni kionjo tu! Kula chuma hicho…!**


---

“Kuna nini mpaka mfunge barabara?” akauliza.
“Leo ni kilele cha sherehe ya Canival, hivo watu wengi watakuwa kwenye hii barabara usiku huu wakisherehekea,” yule askari akajibu na kumwacha Amata huku akielekea upande mwingine kusaidia wengine. Amata akageuza gari lake na kuchukua barabara ile aliyoelekezwa. Ilimchukua dakika kama ishirini na tano hivi kufika eneo analolitaka. Lakini isivyo bahati barabara nyingi zilikuwa zimefungwa kwa hivo ikampasa kuegesha gari pahala pengine.

Akatereka na kujiweka vizuri, kisha akavuta hatua kuelekea upande ambako kelele nyingi za muziki na ngoma zilisikika. Baada ya kupenya hapa na pale, akatokea kwenye hiyo barabara kubwa na kukuta umati wa watu. Mtaa wote ulirindima kwa muziki, ngoma, vinywaji, vyakula na burudani za kila aina. Pamoja na kuwa hapo Antatanarivo kwa siku mbili hakujua kabisa kama siku hii kutakuwa na sherehe hizi kubwa. Akatuliza akili kwanza. Akatia mkono mfukoni na kutoka na karatasi ndogo mkononi mwake.

‘Le Louvre Hotel
7:15PM’

Alipokisoma, akaitazama saa yake kisha akakirudisha mfukoni. Akainua macho yake na




kuiona hotel ile upande wa pili wa barabara. Hivo ilimpasa kuvuka mpaka upande ule na wakati huo umati wa watu ulikuwa umehanikiza barabara yote yaani upande huu na ule kule. Moyo wake ulimwenda mbio maana ni muda mrefu sana hajakutana na kashkash za namna hii. Damu ilipoa. Ilikuwa saa moja na dakika tano usiku alipojitoa pale aliposimama na kujichanganya katikati ya burudani. Lengo haikuwa kuburudika bali kuvuka kuelekea

upande wa pili. Akiwa katikati ya umati ule, alihisi mkono wake ukishikwa na mwingine. Kabla akili yake haijatenda vinginevyo, hisia za mwili wake zilimtuliza. Ulikuwa mkono laini sana ambao mtekenyo wake ulipenya mpaka kwenye chini ya mwili wake. Akageuka na kumtazama huyo aliyemshika. Alikuwa kiumbe mrembo wa kike, macho yake kama binti wa Farao yalimfanya awe mithili ya Cleo Patra. Kiblauzi alichovaa mwilini mwake kilikuwa chepesi lakini kilichoshikamana na mwili wake kiasi kwamba kilifanya matiti mawili ya duara yakae katika mwonekano wa kuvutia. Alikuwa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi.

"Endelea kwenda…" sauti nyembamba na nyororo ya mwanamke yule iliyapenya masikio ya Amata. Akatii. Walipomaliza kuvuka ule umati wa watu na kutokea upande wa pili, yule mwanamke akaongeza mwendo na kumfanya Amata naye afanye vivyo hivyo. Wakalielekea moja ya jengo kubwa lililo jirani na ile hoteli. Mbele tu jengo hilo, yule mwanamke akasimama mbele ya Amata na kumpiga busu la kinywani. "Ina maana warembo hutuoni au? Leo ni siku yetu ya kufurahia maisha na wageni, name nimekuwahi, mwanaume wangu wa leo!" akasema kwa sauti ya kumtoa nyoka pangoni. Kamanda Amata akamtazama upande wa nyuma. Mh! Si mbaya. Kijisketi alichovaa kiliyaacha nje mapaja manene na manono. Kabla hajasema lolote, akavutwa ndani ya lile jengo. Akaingizwa kwenye kambarau na kupelekwa mpaka ghorofa ya tatu. Amata alikuwa kama kondoo anayepelekwa machinjioni. Kimya, mkukumkuku, anaenda tu.

Katika korido ndefu ya sakafu hiyo ya tatu, aliona wanawake wengi na vijana wa kiume katika mikao ya kimahaba. Hapakuhitaji 'D2' kujua kuwa pale palikuwa dangulo. Mlango namba 35 ndipo yule mwanamke akachomeka funguo na kuufungua mlango. Wakaingia ndani na mlango ule ukafungwa. Ndani hapo palikuwa sebule kubwa na nzuri yenya maua kadha wa kadha. Zuria jekundu lilitandikwa kila pahala kisi kwamba hapakua na hata kipande cha sakafu kilichoonekana.

"Njoo!" yule mwanamke akasema huku akiufungua mlango mwingine. Amata akaingia na kukaribishwa na chumba kikubwa chenye kitanda kikubwa, kizuri, chenye nakshi za kila namna. Manukato ya gharama na kila kitu ambacho kingewasukuma wapendanao kuashiriki tendo, kilikuwamo. Yule mwanamke akatupa kipochi chake kitandani, naye akajitupa na kuketi. Upande alioelekeza mgongo palikuwa na dirisha kubwa sana, mapazia yake mawili yalikuwa upande huu na ule na kuacha kioo tu kiasi kwamba aliweza kuona mpaka hoteli ile ya Le Louvre.

"Wewe ni nani?" Amata akafungua kinywa chake kwa mara ya kwanza.

"Usihofu, upo kwenye mikono salama Amata!" yule mwanamke akajibu. Jambo lililokuwa likimshangaza Amata ni lugha. Mwanamke yule alikuwa akiongea Kiswahili safi kisicho na mikwaruzo. Lafudhi halisi kabisa ya Kitanzania. "Kukuleta hapa nimefanya makosa makubwa sana…" akasema. "Makosa ambayo yatagharimu uhai wangu… hata hivyo ni kwa ajili yako," akaongea kwa sauti ya chini lakini ilikuwa 'stereo' kwelikweli.

"Wewe ni nani?" Amata akarudia swali, "Na kwanini uweke maisha yako reheni kwa ajili yangu?" akaongeza swali. Akatazama saa yake, ilitimu saa moja na dakika kumi na mbili jioni. *Bado dakika tatu windo langu lifike!* Akawaza. ***ITAENDELEA***

**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (09)- Na: Eva Mrema

***Ilipoishia…***

**“Napenda watu wanaojiwazia mazuri na kuyachukulia hatua. Pambana, tukijaaliwa uhai, masomo yako Ufaransa yatadhaminiwa na mimi” weeh! Baada ya Sunche kusema hivyo nilimkumbatia na kumbusu shavuni, jambo hilo lilipelekea kila mja eneo lile acheke.**

***Endelea...***

Tulijikuta tumepata marafiki, tulizungumza mengi kuhusu Tanzania, na wao waliongea mengi kuhusu kwao Palestine. Burudani ilipata wafuasi. Tulifundishana michezo mbalimbali, tulicheza na kuburudika. Kiufupi likizo ilileta maana baada ya kuongeza watu wapya maishani wenye uzoefu tofauti. Mi na Sunche tukijikuta peke yetu ni mabusu na mitomasano tu. Yaani aah! Sijawahi kupata raha penzini namna ile. Majira yaliyoyoma. Tulitembea huku na kule. Tulidhuru pori dogo la akiba maeneo yale. Tulikula vya asili na vya kigeni. Tulipiga picha nyingi kama hakutakuwa na kumbukumbu nyingine kama zile.



Siku ya nne tuliitumia kwa mapumziko. Tulikwenda mahali pa singo, tulisingwa na kuingia kwenye mvuke. Tulikoga nongwa zote. Singo yao ilikuwa hatari, ilinukia uturi kuliko ule wa majini. Tulioneshwa kwanini Tanga ndiko yalikozaliwa mapenzi. Tuliifurahia likizo yetu. Kama ilivyo ada, kasi ya usiku mzuri ni sawa na ile ya usiku wa deni, haukawii kukuchwa. Mapema asubuhi tayari tulikuwa garini kuianza safari. Tulihakikisha kila kitu kiko sawa; tulifunga mikanda yetu, haooo! Safari kunoga.

❦

Nilianza kuendesha mimi gari, muziki tuliweka mdogo, mazungumzo yaliendelea. Tulianza kwa kumsakama dogo juu ya maswala ya mahusiano, alibishana nasi hadi hasira kumpata, “Acha kutudanganya mdogo wangu kipenzi, miaka 23 hujawahi kuwa na demu? Huwezi kuwa serious, nitakupeleka hospitali” niliongea huku nikimchungulia kupitia kioo cha juu katikati kinachoonesha sehemu ya nyuma ya gari. Binafsi nilitabasamu, Sunche alicheka na kuomba radhi kwa kuanzisha mada hiyo, baada ya kuona dogo ka-fyumu. “Sitaki mwanamke, hakuna kama wewe dada huko katika pitapita zangu. Nitasubiri wakati sahihi, nitampata wa kuendana na mimi, nataka tu awe na moyo mweupe kama wewe dada na upendo kama marehemu mama”.

Machozi yalinilenga, niliegesha gari kando ya njia kisha nikashuka. Nikafungua mlango wa nyuma na kunyoosha mikono yangu, dogo alikuja mzima mzima nikamkumbatia. “Tobiasi, asante kwa kuwa mdogo wangu. Sijawahi fikiria maisha yangu bila uwepo wako. Naweza kuwa ni mkubwa sana kwako ila tangu tupoteze wazazi wetu, nimekuweka kwenye nafasi ya baba moyoni mwangu. Nakupenda sana, nakuheshimu mno, nakuombea ufanikiwe” niliongea hali machozi yananibubujika. Tuliachiana kwenye kumbatio, Tobi akaushika mkono wangu, “Napenda zaidi unavyoniita Dogo, leo umeniita jina nimeona imekuwa maalumu sana, ukiniita jina nitakuogopa dada”- nikacheka na kumpiga begani na mkono wangu mwingine. “Sijamaliza” akasema dogo. nilimwambia kwa ishara aendelee.

“Asante kwa kuwa mama kwangu, asante kwa kunilea na kunitunza, dada! Cha kukulipa, sitokaa niwe nacho, itoshe kusema tu nakupenda, nakuthamini na ninakuheshimu. Maombi yangu, uwe na furaha wewe” alijipangusa machozi nami


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
‘Offer’ kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (09) - Na: Eva Mrema

nilimkumbatia tena. Tulikumbatiwa kwa juu na Sunche. Alituambia kulia kunatosha. Tulitabasamu huku tunazipangusa nyuso zetu. Tulishuka garini mithili ya watu waliojipanga kuchimba dawa, japo sivyo, tulivuta hewa safi ya msituni. Tayari tulikuwa nje ya mji wa Tanga. Tulirejea garini na safari ikaendelea. Niliendesha gari hadi Moshi ambapo tulipatana kula chakula cha mchana, ingawa ilikuwa mapema. Tulikula kwenye ule mgahawa sababu ya ubora wa mapishi na unadhifu wa mazingira.


Aliyenilogea nguo nyeupe alinipa shida sana, kila nifikapo mahali watu huvutiwa kunitazama. Hali hii mimi huona kawaida kwakuwa najua nguo nyeupe huvutia. Siku hii nilivaa suruali ya jinzi nyeusi na kibode cheupe kilichonishika vizuri na kuifanya namba nane isiyo na kelele kuchongeka vizuri. Nilistaajabu namna Sunche alivyovamiwa na wivu mkali. Mgahawa ule ulihudumia watu wa hadhi ya juu. Kulikaa mibaba upande nyuma ya mgongo wangu. Kumbe kuliendelea uchokozi wa kitamaa tamaa na sikubaini. Nilipoona mabadiliko kwa Sunche wangu, nilimshika mkono na kumuomba tutoke nje.
Tulinyanyuka katikati ya mlo na kutoka nje baada ya kumuona kakasirika na kukosa amani ghafla.
"Mara nyingine hakikisha unavaa nguo zinazoficha mikufu yako ya kiunoni. Vinginevyo vaa gauni, umeona wanaume wanavyotokwa na udenda? Umeona hawa jamaa wanavyonichokoza? Au nikawafundishe namna ya kuwa na adabu kwa mwanamke wa mwenyewe?"

"Basi babaa, usiwe namna hii! Nisamehe mimi nahisi nimeongezeka kidogo hizi siku ndio maana suruali hainikai vyema kiunoni. Nitaenda kwenye gari nikabadilishe" nilimtuliza Sunche baada ya kuona kafura sana na sio kawaida yake. Nilitoka hali akinitazama na kuhisi amenikwaza, japo kiburi kilimshika miguu. Nilisogea mbele kidogo kwenye ukoka nikahisi kuchefukwa vikali. Nilijikaza ila nikashindwa. Ni kama kuna harufu fulani ya ajabu niliihisi ikaharibu mfumo wangu. Nilichuchumaa chini moja kwa moja na hapo niliihisi mikufu yangu ya kiuno ikipulizwa na upepo. Sikujali maana mvurugo niliousikia ulikuwa ule wenyewe.
Nilianza kutapika. Dakika chache Sunche akafika hali ahema; "kumbe bado aliweka lindo bwana" nilijiambia moyoni. Sikutapika sana, ila nilikitoa chakula chote nilichokila pale mgahawani. Sunche alichukua maji garini na kuniletea, nilisukutua kinywa na kisha nilinawa uso wangu maana kuna joto la ajabu nililihisi. Tulielekea garini, Sunche aliwasha kiyoyozi na kunitaka nijitulize. Alitoka kwa haraka na kurejea kule mgahawani. Alilipa matumizi na kumuita dogo. Walikuja wanatembea kama wanajeshi wapya. Sunche akakaa kwenye kiti cha dereva na kusema "tunapita hospitali" nilisisitiza hakuna haja ila hakunisikiliza.
Tulifika kwenye zahanati moja ya binafsi maeneo ya Moshi mjini upande wa pili mbali kidogo tu na stendi ya mkoa. Hakukuwa na watu wengi, haraka tulihudumiwa. Nilionana na dakitari, aliagiza nipimwe vipimo kadhaa. Ndani ya saa moja majibu ya vipimo yalikuwa tayari. Nilimuomba Sunche niingie mwenyewe kupokea majibu. Alimtazama dogo ambaye aliminya macho yake kama ishara ya kumtaka anielewe. Sunche alinipa uhuru. Niliingia na kuketi. Dakitari alikazana sana kusoma kitu kwenye tarakilishi yake. Baada ya dakika kumi nilitoka kwenye chumba cha dakitari. Machozi yalinimiminika. Nililia tu, hata nilipoulizwa sikusema neno. Nilimkumbatia Sunche na kuzidisha kilio.
"Unalia nini ccy? Uko sawa? Una tatizo kubwa?" Mdogo wangu aliuliza wakati huo Sunche alinihimiza kunyamanza kulia ili tuzungumze. "Mpenzi, unataka nikaongee na dakitari? Kuna shida kubwa?" Sunche naye alinisaili.
"Tutapata mtoto! Niliropoka moja kwa moja bila kujali ukubwa na umuhimu wa taarifa niliyoiwasilisha. Sunche alipepesuka na kukalia benchi lililokuwa pembeni yake. Mdogo wangu alinifuata na kuminya mabega yangu kwa nguvu. Alinitazama usoni kisha akaanza kucheka." Sasa dada! ulikuwa unalia nini na wakati mara zote ulitaka sana kuwa mama? Au ndo kilio cha furaha? Maswali ya mdogo wangu, ukimya wa Sunche viliniketisha chini. Kilio kilinipanda kile chenyewe. Nililia mithili ya mama aliyefisha mwana. Sunche alikuja mbele yangu na kupiga goti, hakujali kabisa wapitaji waliofuata huduma pale hospitali. Alinyoosha mikono yake miwili na viganja vyake vikubwa vikalikumbata tumbo langu.

***Itaendelea...***


**BURUDIKA**
www.kitabumarket.co.tz

**KATIKA pitapita zangu huko facebook nikakutana na hivi vipande vya daftari ambavyo ndani yake mumeandikwa hadithi. Baada ya kukaa navyo kwa muda nimemgundua mwandishi wa kazi hizi ni nani. Je wewe umemjua?**




FACEBOOK ni mtandao wa kijamii wenye wafuasi wengi sana. Katika mtandao huu kuna mambo mengi mno, ya kila aina ambayo wafuasi wake huyapadishaili wengine wasome au hata kutazama kwa mtindo wa picha jongefu.

Mimi pia ni mmoja wapo, si ajabu hata wewe umo humo. Nachelea kusema kwamba waandishi wengi wa hadithi na kazi nyinginezo za kifasihi wametumia vyema jukwaa hili kiasi kwamba kwa miaka hii ya karibuni hata wameanza kupata malipokutoka kampuniya META. Na wengi waandishi wa hadithi za Kiswahili wa kizazi hiki wameanzia humu Facebok kuwekakazi zao na kujitangaza kwa wasomaji. Mtandao huu umeleta mapinduzi makubwa sana katikaj jamii hususan vijana wa kileo.




Usiku mmoja katika pitapita zangu mtandaoni kwa minajiri ya kuona nini kimo kizuri au kibaya ndipo nikakutana na picha hizi. Nikaweka tuo na kukodoa ili kuona nini kilichomo. Nikavutiwa na mwandiko, kipande cha simulizi na mpangilio wa wahusika; mpaka picha za wahuzika zilibandikwa kwenye moja ya vipande hivyo kama uonavyo pichani.

Ikabidi nifuatilie kujua ni nani huyu ambaye leo kaamua kuweka wazi ndoto aliyokuwa nayo tangu muda mrefu. Nikajisemea, kama mtuhuyu bado hajachapa kazi yoyote basi anastahili kusaidiwa kwa njia yoyote ile ili afikie kutimiza ndoto yake.

Katika uoekuzi huo, loh! Nakuta kwamba mwenye kazi hizo ni JABALI la kalamu Tanzania. Mmoja waandishi "milionea" wa nyakati hizi. Hakuwa mwingine ila ni mwanadada Laura "Pettie" Kissakwa.

Jamani watu wanatoka mbali sana! Kwakweli nilibaki na vipandehivi nikirudiarudia kusoma "NA WEWE MILELE"

Hongera sana Laura Pettie, sasa tumejua ulipotoka. Hakika ninakuona mbali!



NA WEWE MILELE!

Alipoteremka ndani ya gari na kuanza kuchapua hatua za haraka haraka, kila mtu aligeuza shingo kumtazama, huku wengine wakisimamisha shughuli ili kuyapa nafasi macho yapate kujifurahisha nafsi.

Hakika alikuwa burudani tosha kwa kila binadamu aliyepata nafasi ya kukutana naye. Urefu wake wa kiuanamitindo ulishabahiana vema na umbile lake la wastani lililorembwa zaidi na rangi yake ya senti tano. Nywele ndefu za kimanga ziliangukia mabegani na kuzidi kutoa burudisho bila malipo. Kwa ufupi alikuwa msichana mlimbwende haswaa, ulimbwende ambao si tu hauandikiki karatasini bali pia hausimuliki mdomoni wala kuwazika akilini. Huyu ni Serena Albert Hizza, mtoto wa tajiri Albert Hizza na mkewe Miranda Oluoch raia wa Nigeria. Serena alikuwa afisa uhusiano wa kampuni moja ya simu za mkononi. Alikuwa ni mtoto pekee wa kike kati ya watoto saba wa Tajiri Hizza. Akiwa mtoto wa mwisho Serena alilelewa kama lulu kiasi cha kuwafanya watu waanze kuhisi pengine ndiye mtoto atakayerithi robo tatu ya utajiri wa Mzee Hizza. Katika miaka yake ya ishirini na tatu, Serena hakujua lolote kuhusu kitu shida! Mzee Hizza alifanya lolote kuhakikisha Serena, binti yake anapata kila anachotaka.

Msichana huyu alikuwa amechumbiwa na mtoto wa tajiri mwanamke aitwaye Lady. Kim Kavishe Haroun ndiye haswa aliyekuwa mume mtarajiwa wa msichana huyu mrembo. Kijana huyu tajiri alikuwa Mkurugenzi katika hoteli kubwa ya kifahari iliyokuwa inamilikiwa na mama yake. Alabama Hotel ilikuwa hoteli maarufu na ya hadhi ya juu katikati ya jiji la Dar-es-Salaam. Mapenzi kati ya Serena na Kim yalikuwa yameingia mwaka wa tatu na sasa walikuwa mbioni kuoana, kwa harusi ya kifahari ambayo ilitegemewa kulitikisa jiji na vitongoji vyake



## Tangazo




**Lini ?**

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com